# UBAINISHAJI NA UKOMBOZI WA MWANAMKE KATIKA RIWAYA MBILI ZA K.W. WAMITILA *NGUVU YA SALA* (1999) NA *DHARAU YA INI* (2007)


**MWASILISHI**

**OLUGA JOHN PHILLIP OWADA**


**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**


University of NAIROBI Library
0389592 7


**October 2012**

# UNGAMO

"Tansifu hii ni kazi yangu binafisi na haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika chuo kingine."

31/10/012

Oluga John Phillip Owada

"Tansifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu Cha Nairobi."

31/10/2012

DKT. JAMES OMBOGA ZAJA

1/11/2012

MWL. AMIRI SWALEH

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia baba yangu mpendwa Hayati Silfanus Oluga Owada (1926 – 2011)

Ewe Jehova Mwenyezi,
Bila wewe sijiwezi,
Kanipatia wazazi,
Kwa wema wakanilea.

Baba kwako mkononi,
Ulinitunza makini,
Japo wewe maskini,
Mengi kanikirimia.

Wasia wenye busara,
Tele ulinifundira,
Hata nikawa imara,
Kote ninakopitia.

Kutupatia makazi,
Urithi mwema azizi,

Huo kwetu ni kurunzi,

Mbele kutumulikia.

Hutatoka akilini,

Daima kukuthamini,

Lulu zako maishani,

Ndizo nazitegemea.

Mkono wa buriani,

Tumebaki kwa huzuni,

Kalale pema peponi,

Ukaishi na Jalia.

## SHUKRANI

Katika kuifanikisha kazi hii kuna watu wengi walioniunga mkono; wataalamu jamaa na marafiki zangu. Haikuwa kazi rahisi kuchunguza, kuchanganua, kudadisi na kuandika matokeo ua utafiti wa tasnifu hii. Nijuhudi iliyohitaji wakati, hali na mali ili kuibua tasnifu yenye kina cha mahusiano, ushirika, ushauri, mapendekezo, maelekezo na mawaidha yenye mchango wa fikra nyeti ili kuzalisha ukweli katika uwanda wa akademia.

Kwa mintarafu hiyo, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao, ambao wamenivukisha bahari yenye mawimbi na dhoruba ya usomi kufikia ufuo penye zao la jungu la fikra, dhana, mawazo na kina cha uelewa wa kuzalisha changamoto ya udadisi wa kitaaluma.

Kwanza kabisa, namshukuru Mungu Muumba wa vyote na mwenye uwezo wa vyote duniani na mbinguni kwa uhai na nguvu za kufikia upeo huu wa elimu yangu.

Shukrani zangu za pili ni kwa wasimamizi wangu; Dkt. James Omboga Zaja na mwenzake Mwl. Amiri Swaleh ambao mbali na kuisimamia kazi hii, walinitia shime na kunijaza mawaidha mema ya kitaaluma ambayo yalinisaidia sana katika kufanikisha tasnifu hii.

Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wa Idara ya isimu na Lugha wa Chuo Kikuu cha Nairobi. Hawa ni pamoja na Profesa John Hamu Habwe, Profesa Kyallo Wadi Wamitila, Dkt. Rayya Timammy, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Jefwa Mweri. Dkt. Mwenda Mbatia, Dkt. Iribe Mwangi na Dkt. Mbuthia. Nimefaidika sana kwa mihadhara na mashauri yao ya busara.

Sitawasahau wanafunzi wenzangu wakiwemo Joyce Karinge, Apopo, Nyaga, Watuha, Wanjala, Mburu, Pamela, Margaret Too, Ngunjiri, Mbula, Ngugi na Anjela, miongoni mwa wengine, ambao katika mijadala ya kiusomi tuliyoshiriki pamoja, walinifaa na kunikuza sana kiusomi. Zaidi ya hayo, ninalishukuru darasa zima kwa kuwa nami katika wakati mgumu wa msiba wa mpendwa babangu uliotokea tarehe 4-8-2011, mwishoni mwa kazi yangu. Ninawatakia maisha marefu ya usomi yaliyojawa furaha na ufanisi tele.

Kadhalika nina wingi wa shukrani kwa wazazi wangu wapendwa; Silfanus Oluga Owada, Josefina Aluso Oluga na Monica Achieng' Oluga kwa malezi bora na Shida walizozikabili kwa ujasiri wa kujinyima katika juhudi zao za kunielimisha Katika maisha yangu.

Kisha shukrani za pekee sasa ni kwa mke wangu mpendwa, Mary Anyango Owada na watoto wetu Esther Atieno na Magdaline Akong'o kwa uvumilivu wao ulionipa

moyo na kunielewa katika kipindi hiki cha kozi walipokosa mengi kwa sababu ya gharama kubwa ya kufanikisha kozi hii ya uzamili.

Ninawashukuru marafiki wa dhati kabisa; Jackson Kilaka Aliona, Mandela, Migango, Bw na Bi Alfred Osonga Okelo, Paul Kokelo, George Ouma, Peter Ogol na Dkt Jonyo Fred, Mwl Joseph Ojode wa Nyabisawa Shule ya Msingi na Mwl. Mauris Ojanga Opande wa Kasembo. Shukrani zaidi ni kwa ndugu zangu Rabare Owiti na mkewe Dada Herenia Akinyi, Bi Rose M. W. Akinyi, pamoja na wengine Wote ambao kwa njia moja ama nyingine walinikirimia kimazingira hali na mali Katika muda wote wa kozi hii.

Mwisho ninamtolea shukrani tele, Bi Everlyne Anyango Osoro, aliyetayarisha kazi hii katika tarakilishi yake, kwa kuipigia taipu kwa juhudi na uangalifu mwingi. Alijitolea kwa moyo wote kuichapisha kazi hii katika lugha ya Kiswahili ambayo wapiga taipu wengi huchelea kwa madai kuwa ni ngumu na huchukua muda mrefu. Kwenu nyote, ninawaombea neema na baraka za Mwenyezi Mungu, awape nguvu na afya ya kuwafaa wengine zaidi.

***Kwe mar Ruodhwa Yesu Kristo gi ng'uono mar Nyasaye Nyakalaga obed kodu duto nyaka chieng'. AMEN.***

## YALIYOMO


UNGAMO ........................................ ii

TABARUKU ........................................ iii

SHUKRANI ........................................ iv


## SURA KWANZA


1.0 Utangulizi ........................................ 1

1.1. Tatizo la Utafiti ........................................ 8

1.2. Madhumuni ya Tasnifu ........................................ 9

1.3. Sababu ya Kuchagua Somo Hili ........................................ 11

1.4. Nadharia Tete ........................................ 12

1.5. Upeo na Mipaka ........................................ 12

1.6. Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili. ........................................ 13

1.7. Msingi wa Nadharia ........................................ 15

1.8. Njia za Utafiti ........................................ 22


## SURA YA PILI

## UNAFIKI WA KIDINI NA UKOMBOZI WA MWANAMKE KATIKA *NGUVU YA SALA* (1999)


2.1 Utangulizi ........................................ 23

2.2 Muhtasari wa *Nguvu ya Sala* ........................................ 24

2.3 Mwanamke Kunyanyaswa katika Misingi ya Kidini ........................................ 25

2.4 Wanawake na Mavazi Yasiyokubalika katika Dini ........ 27

2.5 Mafundisho ya Lazima ya Dini ........ 28

2.6 Wanawake na Kicheko kwa Sauti ya Juu ........ 29

2.7 Mwanamke na Uhuru wa Kujitumbuiza ........ 30

2.8 Uchunguwanji wa mwanamke ........ 32

2.9 Mwanamume kama kiongozi wa dini ........ 33

2.10 Mwanamke kubaguliwa kitamaduni ........ 35

2.11 Mwanamke kama chombo cha kufukuzia mikosi ya kijamii ........ 36

2.12 Mwanamke kutengwa na malezi ya watoto ........ 38

2.13 Mwanamke na Suala la Uzazi ........ 40

2.14 Mwanamke Kudhibitiwa Kimabavu ........ 43

2.15 Mwanamke kama Chombo cha Burudani ........ 45

2.16 Suala la Urithi Katika Jamii ........ 47

2.17 Mwanamke Kudharauliwa na Kutukanwa ........ 48

2.18 Majukumu Mengi ya Mwanamke katika Jamii ........ 49

2.19 Jitihada za Kumbainisha na Kumkomboa Mwanamke ........ 50

2.19.1 Mwanamke Kupata Elimu ya Kutosha ........ 51

2.19.2 Kumwamini Mungu Katika Mambo Yote ........ 53

2.19.3 Mwanamke Kupinga Misimamo Mikali ........ 55

2.19.4 Ushirikiano kati ya Jinsia Zote ........ 58

2.19.5 Hitimisho ........ 59

## SURA YA TATU

## UBAINISHAJI WA MWANAMKE NA UKOMBOZI WAKE KATIKA *DHARAU YA INI* (2007)

3.0 Utangulizi ........ 61

3.1 Muhtasari wa *Dharau ya Ini* ........ 61

3.2 Mapendeleo kwa Jinsia ya Kiume ........ 64

3.3 Tamaduni za Kijadi na Ubainishaji wa Mwanamke ........ 66

3.4 Ukatili Dhidi ya Mwanamke ........ 68

3.5 Umaskini na Mwanamke ........ 70

3.6 Mwanamke Kama Chombo cha Burudani ........ 71

3.7 Mwanamke Kama Kiwanda cha Kutengenezea Watoto Wavulana ........ 73

3.8 Uhafidhina wa Wazee na Ubainishaji na Ukombozi wa Mwanamke ........ 74

3.9 Juhudi za Kumbainisha na Kumkomboa Mwanamke ........ 75

3.9.1 Ushirikiano kati ya Wanawake na Wanawake ........ 75

3.9.2 Wanawake Kujiendeleza Kielimu ........ 77

3.9.3 Mchango wa Mashirika ya Ndani na Nje ya Nchi katika Ubainishaji na Ukombozi wa Mwanamke. ........ 79

3.9.4 Mwanamke na Asasi ya Ndoa ........ 80

3.9.5 Ishara za Kimaumbilie na Ukombozi wa Mwanamke ........ 82

3.9.6 Hitimisho ........................................................................ 83

SURA YA NNE

HITIMISHO NA MAPAENDEKEZO

4.0 Utangulizi ........................................................................ 85

4.1 Matokeo ya Utafiti ........................................................................ 86

4.2 MapendekezoYetu ........................................................................ 87

4.3 Hitimisho ........................................................................ 87

Marejeleo ........................................................................ 89

# SURA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Mwanamke ni kiumbe muhimu katika uzao wa mwanadamu. Ndiye msingi hasa katika ukuaji na ukuzaji wa jamii nzima ya kibinadamu duniani. Majukumu ya mwanamke katika familia hayana ubishi kuwa ndiyo nyenzo kubwa katika ujenzi wa familia thabiti. Ithibati hii ndiyo iliyopo katika *Mwisho wa Kosa* ya Z. Burhani tunapomwona Bi. Riziki akiwa mshauri wa bintiye Salama katika familia ya Mzee Bakari.

Masuala yanayohusiana na wanawake, majukumu yao ya kifamilia, kijamii na kitamaduni, nafasi, sauti, mitazamo na ruwaza ya mwanamke katika jamii, ni mambo ambayo yamekuwa katika kitovu cha utunzi wa sanaa tangu jadi. Mwana Rehema katika *Utendi wa Ayubu* anasawiriwa akiwa na majukumu mazito katika kipindi chote Ayubu mumewe alipokuwa mgonjwa. Mwana Rehema katika utendi huu anachukua sifa zote za mwanamke anayewajibika katika familia na kutii sheria za jamii nzima. Mwanamke anahusishwa kwa njia anuwai katika utunzi wa nyimbo, methali, vitendawili, misemo na nahau; na katika nyakati za uandishi ameshughulikiwa katika maandishi kwa njia nyingi. Fasihi mbalimbali za ulimwengu zimemshughulikia mwanamke kwa njia zinazokinzana – baadhi zimemshughulikia kwa njia chanya kama vile Rehema na Bikiza katika *Nyota ya Rehema* ambapo Bikiza anamtafuta Rehema

kwenda kurithi shamba la Bwana Fuad huku Rehema naye akimtafuta Sulubu kwa minajili ya kujenga maisha mema.

Kazi nyingine za fasihi hata hivyo zimemshughulikia mwanamke kwa njia hasi. Tunapata uasi huu kupitia Monika katika *Mwisho wa Kosa*. Licha ya elimu yake ya kiwango cha juu, Monika anakengeuka na jamii yake. Hata hivyo uasi na uchanya ni mambo yanayotegemea utamaduni unaohusika. Tamaduni nyingi za Kiafrika humwona mwanamke kama kiumbe duni anayeishi kwa nguvu za mwanamume kama anavyodai Tripp(2000:17), anapoonyesha jinsi wanawake wa Uganda walivyowekwa mamlakani kupitia nguvu za jamaa zao za kiume. Bell na Offen(1983:16) wanazithibitisha nguvu hizi wanapomnukuu Thomas Jefferson kuwa mwanamume alijaliwa na Muumba wake na haki zisizoaminika juu ya maisha, uhuru na ufuatiliaji wa furaha, ilhali baadhi ya tamaduni zizo hizo za Kimagharibi hupigania usawa wa jinsia kwa kumtetea mwanamke. De Beauvoir (1949) na Millet (1969) wameandika kwa mapana na marefu kuitetea jinsia ya kike licha ya kupigania usawa wa jinsia zote.

Katika fasihi andishi ya Kiswahili, mwanamke ameshughulikiwa kwa njia changamano – kama mama na mlezi, kama mke na mpenzi, kama mhimili wa familia, kama mwasi na mgonganishaji, kama kahaba na mvunja maadili, kama kiumbe cha binadamu anayedhulumiwa, kuonewa na kudhalilishwa,

mwanamke kama mwathiriwa wa asasi za kijamii au hata mwanamke kama mfadhiliwa wa asasi za kijamii. Fasihi zinazowadunisha wanawake zimepingwa na vyama vya wanawake katika nchi za Afrika kuanzia Afrika Kusini, Nigeria, Kenya hadi Uganda(Tripp 2000;14).

Mfano wa mwanamke kama mama na mlezi unajitokeza katika *Nyota ya Rehema* tunapomwona Bikiza akimchukua Rehema, baada ya kifo cha mamake, na kumfuata baadaye akimtafuta akadai urithi wa shamba la Ramwe alikozikwa mamake, Aziza. Usawiri wa mwanamke kama mpenzi unajitokeza kwake Mwana Rehema wa *Utendi wa Ayubu* pale anapomshughulikia mumewe Ayubu kwa hali na mali alipopatwa na ugonjwa wa ukoma. Alifanyiwa fitina nyingi ili amwache mumewe lakini alibakia mkewe Ayubu hadi mwisho. Mama Mtu-Maanani wa *Walenisi* ni kielelezo cha mwanamke kama mhimili wa familia. Tunapomwona akitoa ushauri mzito kwa kila mmoja katika familia walipotembelewa na Dzombo. Bi Farashuu wa *Utengano,* tunapomwona akiwagonganisha Bi. Tamima na Maksuudi, Kadija, Maksuudi na Mussa katika riwaya nzima. Tabia ya umalaya na uvunjaji maadili inajitokeza katika kazi ya Kezilahabi kwao Tegemea na Nyabuso wa *Kichwamaji.* Tunaelezwa hapa kuwa Tegemea alipokuwa bado mwanamwari alifanya kazi ya umalaya. Nyabuso anachukua suruali ya Kazimoto kwa kukosa kumkidhia haja yake usiku. Mwanamke anaonewa, anadhulumiwa na kudhalilishwa katika *Utengano* inavyojidhihirisha kupitia Tamima na

Maimuna bintiye. Ingawa *Utenzi wa Kiokozi cha Banati* wa Sheikh Mohamed Jambeini unaegemea dini ya Kiislamu, sheria zilizopo zinaonekana kama ni za kitamaduni. Katika ndoa, mke anatakiwa kumnyenyekea mumewe, kumpumbaza kwa kumpepeta, kukaa eda akifiwa na mume na kutomsogelea mume nyakati za hedhi. Huku ndiko kumfanya mwanamke mwathiriwa wa asasi za kijamii na kuwa mfadhiliwa wa asasi hizo. Hali kama hizi ndizo zinamfanya mwanamke kuonekana daima kama msimamizi wa utamaduni(Turshen na Holcomb1993:xvi) na pia zinavyodhihirika kwao Nzisa (*Nguvu ya Sala)* na Kasina(*Dharau ya Ini)*.

Uchanganuzi wa jinsi wanawake wa Afrika hujichukua na kuauni kigezo cha tamaduni zao, huzingatia matatizo anuw ai yanayowakabili katika vita mfululizo vya mipaka ya kiuchumi na siasa wanayowekewa kwa kudhulumiwa kijinsia na kitofauti za rangi (Terborg-Penn1989:xii-xiii). Mbinu hii itapelekea uelewa wa mandhari ya utamaduni na kukubali ubainishaji wa wanawake wenyewe na jinsi wanavyojidhihirisha(xv). Wanawake wa Afrika wana nafasi finyu katika nyadhifa za kidini sawa na wenzao weusi katika nchi ya Marekani.

Imani kubwa katika bara la Afrika ni kwamba mwanamke hukamilika kupitia uwezo wake wa kuzaa na kuwalea watoto pamoja na familia yake. Taratibu hizi za kidesturi huwa na nguvu na si rahisi kuzivunja bila ya kanuni za kimataifa juu ya haki ya jamii (SIDA2009:68,75). Hapa ndipo hati na mikataba

ya kimataifa kama vile Protokoli ya Haki ya Binadamu kuhusu wanawake wa Afrika tunayoielezea katika msingi wa nadharia hapo baadaye katika sura hii huingilia. SIDA (2009) inashauri kuwa vyombo vya dola vinafaa kuielimisha jamii na ili wanawake wajiwajibishe katika masuala yanayowahusu kimaisha.

Tahakiki za akina Lugano (1980), Mwangangi (1996) na Musyoka (2007) hazikugusia ubainishaji na ukombozi ndipo tukapata pengo la kujaza ambalo ni ubanishaji na ukombozi wa mwanamke. Ubainishaji ni dhana tunayoitumia kwa maana ya kumpa mwanamke utambulisho wake, akubalike na kuchukuliwa kwa mtazamo chanya katika jamii. Dhana ya ukombozi ina maana ya uokoaji wa watu kutoka kwenye hali mbaya ya udhalimu au hali duni. Haya ni matatizo ya tajriba kwani mwanamke hana haki ya kurithi mali, kutoa maoni na daima anachukua amri kwa mwanamume (Tripp 2000:30). Tutajikita katika uhakiki wa kinadharia wa kifeministi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003:253) ufeministi ni nadharia ambayo imeweka msingi na msukumo mkubwa pamoja na nia ya kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Tutaegemea mtazamo wa ufeministi wa kiharakati katika kuhakikisha ubainishaji na ukombozi wa mwanamke katika kazi mbili za Wamitila; *Nguvu ya Sala* (1999) na *Dharau ya Ini* (2007). Kulingana na Wafula na Njogu (2007), ufeministi wa kiharakati humchukua mwanamume kama adui mkubwa

wa mwanamke. Mkondo huu unaamini kuwa uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio hutumiwa na mwanamume kumdhalilisha na kumtawala mwili wake. Kama tulivyoelezea hapo juu, ubainishaji unatumika kumaanisha kumpatia mwanamke utambuzi katika jamii na kumtofautisha na jinsia ya kiume. Kwa upande mwingine, ukombozi utatumika kumaanisha matendo au harakati za kumwokoa mtu kutoka kwenye hali mbaya ya mateso na unyonge. Taratibu za imani za kitamaduni ziliratibishwa na fasiri za kiume na mikabala ya kiubabedume. Madai haya ni kwa mujibu wa Turshen na Holcomb (1993;xviii) wanaposema kuwa kuanzia nyanja za kimataifa na za kimaeneo, sera za umma huratibishwa hasa na wanaume na kwa njia mbalimbali waathiriwa huwa ni wanawake na watoto. Taratibu hizi zinamfanya mwanamke akose haki na kuonekana mnyonge mbele ya mwanamume. Tumechagua mtazamo huu wa ufeministi wa kiharakati kwa msingi wake wa kupinga mfumo wa kiubabedume unaomwonea mwanamke katika asasi zote kuu za kijamii kama ndoa, dini, siasa na uchumi.

Mwamko wa kiharakati wa wanawake kupigania haki zao umezuka tangu mwaka wa 1818 kwa njia ya maandishi na Mary Shelley katika riwaya yake inayojulikana kama *Frankenstein*. Harakati hizi zilishika moto katika enzi za Malkia Victoria kati ya miaka ya 1830 – 1930. Millett (1969: 62) anaelezea kipindi hiki kuwa, "Ni muhimu kukumbuka kama wakati wa ukandamizwaji wa kijinsia kwa madai ya kuwa na adabu ulifikia upeo wa mgogoro, na kuwa

ni njia moja tu ndiyo iliwezekana – faraja." Hii ilimaanisha kupatikana kwa kiasi cha uhuru wa kijinsia kwa wanawake, kikundi kilichonyimwa mengi kama vile ukosefu wa hadhi katika jamii. Wanaharakati Elaine Showalter (1977), anaonyesha historia ya harakati hizi tangu mwaka 1840 kwa njia ya maandishi kuhusu wanawake. Watetezi wengi wa nadharia hii walikuwa wanawake wenye ithibati tosha kuwa jitihada za ukombozi wa wanawake zimeendelezwa sana na wanawake wenyewe. Baadhi yao ni kama vile Virginia Woolf (1929) katika kazi yake; *A Room of One's Own* (1929) na Mary Wollstonecraft (1972) alipoandika *A Vindication of the Right of Women.*

Simone de Beauvoir (1949), mwananadharia wa Kifaransa, amebainisha, amekosoa na kupiga vita asasi zinazomdhalilisha na kumdunisha mwanamke. Dini imetumika kumkandamiza na kumfundisha mke kumnyenyekea mumewe katika hali zote. Ndoa nayo inampa mwanamume uwezo juu ya mwanamke ikizingatiwa kuwa mume ndiye mkuu wa familia, kiongozi wa dini huku mwanamke akikosa nafasi maalumu katika huduma za kidini. Hali kama hizi zinamfanya mwanamke abakie katika nafasi ya chini na kuonekana kiumbe duni mbele ya mwanamume kwa hivyo kuibua haja ya kupigania ubainishaji na ukombozi wake.

Kama anavyoeleza na kufafanua de Beauvoir, mtazamo huu sasa umepitwa na wakati. Mwanamke ni sharti sasa apewe nafasi sawa na mwanamume katika

kutekeleza majukumu maalumu ya kijamii. Ni katika mtazamo huu ndipo tumepata pengo la kumbainisha mwanamke na wala sio tu kumkomboa kutokana na dhuluma na fedheha anayokumbana nayo katika maisha yake. Hapa ndipo tunapogundua kuwa tapo la pili na la tatu ya ufeministi yaliyozuka kati ya miaka ya 1960 – 1990 yana majukumu maalumu. Wakati huu wanawake wenye elimu na walioko katika tabaka la kadri walipigania kutokuwa sawa kitamaduni na kisiasa. Ili kufanikisha lengo hili, tumependekeza ufeministi wa kiharakati kama mtazamo utakaotawala katika uhakiki. Ufasiri wa nadharia hii unapatikana kwa kina katika msingi wa nadharia kwenye sehemu zinazofuatia. Haya ndiyo masuala tunayoshughulikia ili kupatikana suluhisho mwafaka ya ubainishaji na hatimaye, ukombozi kamili wa mwanamke tunayemrejelea hapa. Mwanamke anastahili hadhi maalumu sawa na mwanamume ili yapatikane maendeleo katika mazingira husika.

## 1.1. Tatizo la Utafiti

Katika kazi hii tulishughulikia ubainishaji na ukombozi wa mwanamke hasa kwa kuzingatia uumbaji na usawiri wake katika fasihi ya Kiswahili kama unavyojitokeza katika kazi mbili za Kyallo Wadi Wamitila, *Nguvu ya Sala* (1999) na *Dharau ya Ini* (2007). Tulichunguza jinsi mifumo ya kijadi ya kiuchumi, kisiasa, kidini na kijamii inavyotumiwa na mwanamume kumkandamiza mwanamke.

Utafiti wetu pia ulidadisi jinsi mwandishi wa kazi hizi tulizozichagua, anavyoshughulikia maovu anayotendewa mwanamke na juhudi za kiharakati zinazogusiwa na mwandishi kuwasaidia wahusika wake wa kike ili kujinasua kutoka kwenye minyororo ya udhalimu, ukandamizwaji na unyanyaswaji mkononi mwa mwanamume. Tunataja udhalimu hapa kwa maana ya tendo la kutesa, kuonea, ukatili na mambo anayotendewa mtu kinyume na haki anayostahili kutendewa.

Kadhalika tulitathmini taswira za mwanamke kama kiumbe katika fasihi au katika jamii hasa kwa kiulinganisha na jinsi wahusika wa kiume wanavyochukuliwa katika mazingira yale yale. Hali hii ilituelekeza kuhakiki jinsi mwanamke anavyojichukusa katika fasihi au katika jamii tukizingatia changamoto zinazomkwamisha mwanamke yuyu huyu katika maendeleo yake kwa ujumla. Kisha tulitoa mapendekezo yetu ambayo yanaweza kusaidia kukomesha udhalimu unaomkumba mwanamke ili kumbainisha na kumkomboa atoke kwenye udhalili na udhia aliomo katika jamii.

## 1.2 Madhumuni ya Tasnifu

Lengo la kimsingi la utafiti huu ni kumulika mahusiano yaliyoko katika ubainishaji na ukombozi wa mwanamke tukimlinganisha mwanamke wa fasihi na mwanamke katika maisha halisi ya kijamii tukizingatia masuala ya maendeleo, uhamasishaji, malezi, haki za kibinadamu na mahusiano yake na

asasi mbalimbali za kijamii. Katika hali hii, tuliangalia jinsi mwanamke anavyokandamizwa na kunyanyaswa na juhudi zinazoonekana katika riwaya hizi za kumbainisha na kumkomboa mwanamke.

Kufuatia mwamko wa kisasa wa kuzipigania haki za mwanamke, utafiti wetu ulijishughulisha na jinsi asasi za kijamii na kihistoria, zilivyotumika vibaya kumbagua, kumtenga na kumdhalilisha mwanamke na kwa njia hiyo kumnyima haki zake. Hali hizi ndizo zinamfanya mwanamke kuchukuliwa kama kiumbe duni anayemnyenyekea, anayemtii na kumtegemea mwanamume kwa kanuni za asasi zilizoratibishwa kwa upendeleo wa kiume.

Tulipitia mijadala mbalimbali ya kiusomi kudhihirisha maudhui ya tamaduni tofauti tofauti na jinsi zinavyomuumbua na kumdunisha mwanamke, jinsi tofauti za kijamii, historia na tamaduni tofauti za kiusomi na upokezi wake na hadhira zenye matarajio mbalimbali. Ili kufikia malengo haya, utafiti huu ulilenga kutumia ufeministi wa kiharakati kama msingi wa nadharia ya kuonyesha jitahada ambayo mwanamke anafaa kufanya na mikakati ya kupinga maonevu hayo yanayomkumba mwanamke maishani. Hii ndiyo sababu tulitumia mtazamo chanya unaojitokeza katika kazi hizi za *Nguvu ya Sala* na *Dharau ya Ini* kama jitihada za ubainishaji wa ukombozi wa mwanamke ili kuwa kielelezo mwafaka cha kuthibitishia mada tuliyochagua kumtetea mwanamke. Tuliangalia jinsi mwanamke na wahusika wengine

wanavyochangia harakati za ukombozi huu kupitia matendo yao na jinsi wanavyotagusana katika kutekeleza ubainishaji na ukombozi kamili wa mwanamke.

## 1.3. Sababu ya Kuchagua Somo Hili

Matapo ya pili na la tatu ya Ufeministi yaliyozuka kati ya miaka ya 1960-1990 yana majukumu maalumu. Wakati huo wanawake wenye elimu waliokuwa katika tabaka la kadri, walipigania kutokuwapo usawa wa kitamaduni na kisiasa.

Ili kufanikisha lengo hili, tulipendekeza ufeministi wa kiharakati kama mtazamo wetu katika uhakiki wetu huu. Fasiri ya nadharia hii inapatikana katika msingi wa nadharia kwenye sehemu zinazofuatia. Haya ndiyo masuala tunayoyashughulikia ili kupatikana suluhisho mwafaka ya ubainishaji na hatimaye, ukombozi wa mwanamke tunayemrejelea hapa.

Mwanamke anastahili hadhi maalumu sawa na mwanamume katika kujiendeleza katika mazingira husika. Kwa hivyo, tulichagua kushughulikia ubainishaji na ukombozi wa mwanamke kwa pamoja, ili kujaza pengo linalojitokeza katika tahakiki tangulizi za riwaya za kisasa zaidi zinazokabiliana na hali za kisasa zinazomkumba mwanamke. Tulionelea tuchague riwaya zilizo na usimulizi unaopitia sauti ya mwanamke ili kupata

picha kamili ya matatizo yake na kutumia hali hiyo kuunga mkono upya, yaliyoibuka kwa kupigania haki na usawa wa mwanamke na mwanamume katika jamii tuliyomo.

## 1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatayo:

(i) Asasi mbalimbali za kijamii huwachukulia wanawake kama mapambo na chombo cha burudani cha kutoshelezea ashiki za mwanamume.

(ii) Mwanamke huchangia kwa kiasi fulani unyanyaswaji na ukandamizwaji wake na jinsia ya kike kwa ujumla.

## 1.5 Upeo na Mipaka

Tasnifu hii ni uhakiki wa kifasihi na tulijifunga katika riwaya mbili za Wamitila, *Nguvu ya Sala* (1999) na *Dharau ya Ini* (2007). Kazi hizi tutazitumia kushughulikia masuala ya ubainishaji na ukombozi wa mwanamke. Tuliangalia jinsi mwandishi alivyowaumba na kuwasawiri wahusika wake wa kike na nafasi zao za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kielimu anazowapa.

Katika kufanya hivyo tulitumia mtazamo wa ufeministi wa kiharakati na kuzingatia uhakiki wa kimaudhui.

## 1.6. Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili.

Kamande (1983) akihakiki wahusika wa kike katika riwaya ya *Utengano* ya S. A. Mohamed, anasema kwamba, mwanamke amewekwa katika kundi la wanyonge kwa kudhulumiwa na kudunishwa anaponyimwa sauti na mwenye nguvu. Ingawa kazi hii inajikita katika maudhui ya riwaya tatu za S. A. Mohamed, *Utengano, Dunia Mti Mkavu* na *Asali Chungu*, inaonyesha jinsi mwanamke anavyokandamizwa na mifumo ya kiubabedume, uhakiki wake ni tofauti na wetu unaojishughulisha na ubainishaji pamoja na ukombozi wa mwanamke. Kwa hivyo, Kamande alipotafiti kazi hizi alilenga kuonyesha njia mbalimbali anazodhulumiwa mwanamke kwa kuzijadili na kuzikosoa. Hakufaulu vyema kwani hakutoa mapendekezo yanayotufaa hapa kwani aliegemea zaidi fani wakati utafiti wetu unajishughulisha ubainishaji zaidi na ukombozi wa mwanamke.

Ndungo (1985) amejishughulisha na maendeleo ya mwanamke kihistoria kwa mtazamo wa U-marx na kumwona kama kiumbe duni ambaye ameshurutishwa kudunishwa katika mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi, na kuchukua nafasi ya nyuma baada ya mwanamume. Kazi hii, "Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili," ni muhimu kwetu kwani imetilia maanani matatizo mengi ya wanawake ambayo aghalabu husababishwa na maingiliano ya kijamii baina yao na wanaume. Mtazamo huu ni tofauti na wetu kwani Ndungo anatumia mtazamo wa U-marx huku kazi yetu ikiegemea

kitengo cha ufeministi wa kiharakati. Hata hivyo, tunakubaliana na Ndungo kuwa msingi wa kuonewa kwa mwanamke ni taratibu za mifumo ya kijamii zilizomjengea mila na desturi zinazomdhalilisha, zinazomfanya kudharauliwa na kumweka daima katika nafasi ya chini akilinganishwa na mwanamume. Hakuna hata moja kati ya kazi tulizozitaja hapo juu inayojishughulika na ubainishaji wa mwanamke japo zimegusia ukombozi wake kwa kutumia mitazamo mbalimbali. Utafiti wetu kwa hivyo, una nafasi ya kujaza pengo hilo tulilolitaja.

Lugano (1989) amehakiki nafasi ya mwanamke katika jamii ya kitabaka. Katika kazi hiyo, "Mwanamke katika riwaya za Kezilahabi," amebaini jinsi mwanamke anavyojitosheleza kama mzazi, chombo cha kumfurahisha mume, chanzo cha maovu ya kila aina na mtumwa wa mwanamume. Ingawa mtazamo wake unaelekea kuwa sawa na wetu, sisi tulishughulikia ubainishaji na ukombozi wa mwanamke ili ajinasue kutoka kwa minyororo inayomtweza katika mazingira yake. Hata hivyo, kazi ya Lugano imechangia kutuonyesha jinsi jamii zinavyomdharau na kumkandamiza mwanamke na kumnyima nafasi zote za uamuzi katika baadhi ya shughuli, kama si zote za jamii husika.

Mutua (2007) katika kazi yake; "Mitazamo ya vijana na Wazee Kuhusu Ukombozi wa Mwanamke katika Tamthilia Tatu za Kiswahili," anashughulikia mchango wa vijana na wazee katika ukombozi wa mwanamke. Anajadili njia

mbalimbali ambazo kwazo mwanamke amekandamizwa katika jamii. Kazi hii, "Mitazamo ya Vijana na Wazee kuhusu Ukombozi wa Mwanamke katika Tamthilia Tatu za Kiswahili", ni muhimu kwetu kwani inahusu mada yetu lakini inamulika mada tofauti kidogo kwani kazi hii haigusi chochote kuhusu ubainishaji wa mwanamke.

### 1.7. Msingi wa Nadharia

Nadharia tuliyoichagua kushughulikia mada yetu ni ufeministi wa kiharakati. Dhana ufeministi inatokana na neno la Kilatini "Femina" linalomaanisha mwanamke. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2000), ufeministi umefasiriwa kama tapo la kupigania ukombozi, haki na usawa wa wanawake; yaani nadharia ya usawa wa wanawake. Kwa hivyo, ufeministi ni dhana ya kihakiki inayolenga kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na vizuizi vya kitamaduni, kidini, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Wanaufeministi walijumuisha athari za kisaikolojia zinazowahusu wanawake kupitia mateso katika jamii zinotwaliwa na wanaume.

Ufeministi wa kiharakati unashikilia msingi wa tofauti za kijinsia ambapo chanzo cha ukandamizwaji unathibitisha kuwa mwanamume ndiye mwenye mamlaka makuu ya uwepo wa mwanamke. Huu ndio msingi wa wanaume kunyakuwa uwezo wote juu ya mwanamke (Mary Eagleton 2007:159/160). Msingi huu ndio unaomfanya Millett (1969) kutofautiana na mawazo ya Freud

ambayo kwa kipindi kadha yanasisitiza utaasubi wa kiume dhidi ya mwanamke (Eagleton:161). Kwa upande mwingine Millett naye anaziona ithibati hizi kama njama za Freud kudumisha ubabe wa kiume kwa kumfunga mwanamke katika jukumu lao la umama pekee. Isitoshe, madai kuwa ridhaa ya mwanamume kwa mwanamke kuwa ni kuzaa ni ishara tosha ya kumfanya mwanamke kuwa chombo tu, na katika hali hiyo anadunishwa (Millett:185). Hivyo basi, nadharia hii inamchukulia mwanamume kama kiumbe anayemwonea mwanamke kupitia asasi za kijamii tulizozitaja hapo juu; kidini, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi.

Kwa mujibu ya Wafula na Njogu (2007), waitifaki wa mkondo huu wanaamini kuwa uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio hutumiwa na mwanamume kudhalilisha na kumtawala mwili wake. Kwa hivyo, wanaufeministi wa kiharakati wanamchukua mwanamume kama adui mkubwa zaidi wa mwanamke. Hivyo basi, ili wanawake waweze kujitawala katika nyanja zote za maisha, wanahimizwa "wasiolewe na mwanamume!" Sio kutoolewa tu, bali wanawake washirikiane wao kwa wao ili kupambana na taratibu zilizowekwa na mwanamume kumdunisha mwanamke (Tripp:2000).

Wanawake walidhihirisha ukakamavu wao wakati suala la ufeministi ulipoibuka tena kama vuguvugu ya kisiasa katika nchi za Kimagharibi miaka

ya 1960 na kuwa na msimamo thabiti ya kupigania haki zao bila woga ( Moi 2002:21).

Wamitila alipoziandika kazi hizi, mwamko mpya wa kiharakati ulikuwa umeshazinduliwa Barani Afrika kupitia Protokoli ya Haki ya wanawake wa Afrika na ya Haki za Binadamu kuhusu Haki za wanawake wa Afrika mwanzoni mwa 2000 inayovipa vyombo vya dola wajibu katika haki za afya, ujinsia na uzazi wa wanawake. Kwa kuwachora wahusika wake katika vitabu tulivyovihakiki, msanii anaeleza kwamba kila jamii ina kanuni zake ambazo kwazo kitendo chaweza kuonekana sawa au si sawa.

Hata hivyo, tapo la pili lililoishia mwaka 1920 ni lile ambapo wanawake walijiundia upinzani na hasa uliokuwa ukiwasilisha masuala ya madai ya kike. Hii ilikuwa kubadilisha mtindo wa miaka ya 1840 hadi 1880 ambapo wanawake wengi waliandika kwa kuiga mitindo ya kiume kutilia maanani mawazo ya kike .

Tapo la tatu la tangu 1920 hadi sasa , maandishi ya wanawake yanajikita katika uvumbuzi nafsia na uchunguzi wa ndani wa uzoefu wa wanawake katika kupigania haki zao. Hili ndilo tapo ambalo linatufaa kwani nadharia tuliyoitumia inalenga kumkatia mwanamke ubainishaji kamili katika jamii kwa kuzikosoa itikadi zilizopitwa na wakati .

Millett kadhalika anayapinga mawazo ya Freud kuwa itikadi za kiume ziliwekwa na mwanamume mwenyewe kuthibitishia ujarabati wa usawa wa hadhi za wanawake (Eagleton:162). Kwa mujibu wa Millett, umbo la mwanamke unadhirishwa na jukumu la ujinsia wake (Millett 1969:202). Siasa za kijinsia zilifikia awamu mpya mwishoni mwa miaka ya 1960.

Ufeministi wa kiharakati unapinga hali ya kuwa mahusiano ya kijinsia hutegemea sheria na mila za kienyeji kuliko desturi za kawaida. Hali hii impelekea Eva Figes kudai kuwa wanawake kwa muda mrefu , wamekuwa viumbe waliotengenezwa na binadamu kinyume na walivyo wanaume. Tunalishutumu wazo hili kwani ndilo sababu mara mingi wanaume wanawachukulia wanawake kuwa sehemu ya mali yao. Kwetu, viumbe wa jinsia zote ni sawa na hivyo mwanamke anahitaji kubainishwa kikamilifu ili afikie ukombozi bila bughugha za kudhulumiwa kila wakati.

Kanuni za kihistoria zinasisitiza jinsi mapatano ya umma yamekuwa yakiendeshwa na wanaume na hali ya kuwa mwanamke huengemea manufaa ya mwamume . Kwa kuwa kiumbe mwenye nguvu, mwanamume ndiye aliye na haki ya kufanya kitendo cha kinyumba huku mwanamke akihusishwa kimwili tu. Ni wanaume pekee ndio wenye haki ya kutumia nguvu ilihali wanawake ni viumbe wa kulalamika kwa sauti ya juu tu! Ni kupitia dai hili

ndipo tunaona ya kuwa, ni bora mwanamke apate nafasi sawa na ya mwanamume katika jamii ili atambulike kuwa ana sehemu yake ya kuchangia katika maendeleo ya uzalishaji mali katika umma .

Wananadharia hii wanalenga kutilia mkazo kuwa wanawake waliwekwa katika uraia wa nyumbani wakati wanaume wakiwekewa umuhimu katika mawanda ya kiuchumi, kisayansi, kisanaa na kisiasa (Sylvester1994:24). Mwananadharia huyu, Sylvester, anamnukuu Boxer na Quataert (1987) wakisema kuwa mageuzi ya kisayansi yaliyostawi katika karne ya kumi na saba kwa kiasi kikubwa yalikuwa mambo ya wanaume. Hata hivyo wanawake wachache walishiriki na kupendekeza upangaji upya wa mamlaka ya kinyumbani ili kuboresha nafasi ya jinsia ya kike.

Njia za kuwafanya wanaume kuchukuliwa kuwa ndio bora kuliko wanawake, ndiyo imepelekea mifumo mingi kidesturi na kisheria kuwa na tamaduni anuwai ya wanawake kudhurika katika dhuluma za mwanamume (SIDA 2009:60).

Kwa hivyo, fikira za Millett kuhusu ufeministi wa kiharakati ni kuhamisha ugumu wa kufahamika usiopendeza wa ukandamizwaji wa wanawake kwa kuwatenganisha kijinsia katika majukumu ya kawaida katika jamii. Mwanamume huweka masharti ya kiakili katika ukandamizwaji wa wanawake

ambayo ndio msingi wa wanawake kudhulumiwa (Eagleton:163-164). Akimnukuu Mary Daly (1973), Eagle anadai kuwa historia ndefu imethibitisha kuwa udhalili wa wanawake chini ya mwanamume ni utaratibu uliofutilia mbali suala la wanawake kiasi kwamba hata wanawake wenyewe hawana uwezo wa kusikia wala kueleza kwa usahihi suala linalowahusu katika maisha yao ya kawaida (Eagleton2007:5).

Unyanyaswaji humnyima mwanamke uhuru wake kufuatia dhuluma kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiitikadi. Sharti wanawake washughulikie mageuzi bila uzembe wa kuzifanya kuwa ni hali zao ya kawaida maishani (Moi 2002:178). Moi anapendekeza zaidi kuwa, ili kuepukana na madhihirisho ya kimsingi na ya kibiolojia, inabidi wanawake wakatae wazo kuwa maumbile kibiolojia ndiyo hufanywa kanuni za jamii. Kasumba ya mawazo kuwa wanawake hawawezi kujifanya waeleweke kwa kuwa wanyonge haiwezi kufaa cho chote katika ukombozi wao( 178,179).

Moi anapomnukuu Simone De Beavoir anadai kuwa mwanamke ni "mtu mwengine" wa mwanamume; kinyume chake au taswira geu (kioo) ya mwanamume (Moi2002:133). Katika madai haya tunakubaliana na De Beavoir kwani katika tamaduni za wanaume mwanamke anaonewa na kukubalika tu kama "mtu mwengine" wa mwanamume. Hii ndio sababu Irigaray alivyonukuliwa na Moi, anadai kuwa mahubiri ya mwanamume

yanamweka mwanamke nje ya uwakilishi kuwa hayupo, ni kanushi, bara jeusi ama kwa wema zaidi, mwanadamu duni! (Moi 2002:133).

Wananadharia ya kiharakati, akiwemo Kate Millett, walitumia maandishi yao kama njia moja ya kuwatahadharisha na kuwatanabaisha wanajamii kuhusu maovu ya kuidharaulia mbali jinsia ya kike.

Kwa kutumia ufeministi wa kiharakati, tulichanganua namna mbalimbali ambavyo mwanamke anadhulumiwa katika jamii ya kimaandishi na kuonyesha juhudi zilizotumiwa na mwandishi kumbainisha na kumkomboa. Hii itasaidia katika kupelekea ubainishaji na hatimaye ukombozi kamili wa mwanamke.

Kwa mujibu wa Kratochril (1974) kufikiria ukombozi wa wanawake wa Afrika ni suala lililotokana na mambo yanayohusu mihemko ya ukombozi wa wanawake katika nchi za Marekani na Uropa. Tangu zamani wanawake wameshushwa hadhi hadi kiwango cha chini. Nadharia hii ya ufeministi, kimsingi, inapigania usawa wa binadamu na inaonyesha udhaifu wa mfumo wa kiubabedume. Mkondo huu unatetea uhuru wa mwanamke kwa kudai kuwa ana haki ya kufurahia haki zote za kibinadamu sawa na mwanamume. Tuliitumia mkondo huu wa kifeministi kuchanganulia njia zote za udhalimu anazowekewa mwanamke kama mchango wa kusaidia katika ubainishaji na hatimaye ukombozi wa mwanamke.

Kwa kutilia maanani mawazo haya, tulitumia nadharia ya ufeministi wa kiharakati katika kuhakiki kazi mbili za Wamitila; *Nguvu ya Sala* (1999) na *Dharau la Ini* (2007).

**1.8. Njia za Utafiti**

Njia yetu ya kwanza ni kuzisoma kwa kina riwaya tunazozishughulikia kwa mtazamo wa kifeministi ili tupate mtazamo kamili wa mwandishi kumhusu mwanamke anayemsawiri na kumwasilisha katika riwaya zote mbili. Utafiti wetu utakuwa wa maktabani. Tulipitia na kurejelea maoni ya wasomi waliochangia masuala yanayohusu mada yetu ili tupate mwelekeo unaofaa. Kwa mujibu wa Kratochril (1974) kufikiria ukombozi wa wanawake wa Afrika ni suala lililotokana na mambo yanayohusu mihemko ya ukombozi wa wanawake katika nchi za Marekani na Uropa. Tangu zamani wanawake wameshushwa hadhi hadi kiwango cha chini.

# SURA YA PILI

# UNAFIKI WA KIDINI NA UKOMBOZI WA MWANAMKE KATIKA *NGUVU YA SALA* (1999)

## 2.1 Utangulizi

*Nguvu ya Sala* (1999) ni kazi ambayo inaonyesha jinsi dini inavyotumika vibaya kumnyanyasa mwanamke. Unafiki ni hali ambayo mtu hujifanya mwema huku akisema au kutenda kinyume na hali inavyoaminika. Unafiki uliopo unaashiria namna ambavyo mwanamume anatumia asasi ya dini kumfanya mwanamke kuonekana duni na asiye na thamani katika imani za kiroho na kubakia chini ya utawala wa kimabavu wa mwanamume. Ufeministi wa kiharakati tunaoutumia katika tasnifu hii ni mtazamo unaozingatia harakati za mwanamke kujinasua kutoka katika minyororo aliyowekewa na jamii yenye mfumo wa kiubabedume na kuiwekea jinsia ya kike vizingiti vingi vya kitamaduni, kidini, kisiasa na kiuchumi.

Sura hii itashughulikia juhudi zote zinazofanywa na wahusika wa kike na wa kiume kumnusuru mwanamke kutokana na hali ya kukandamizwa. Kadhalika tutajadili jinsi mwandishi ameifanya elimu kuwa chombo muhimu cha kumkomboa mwanamke kutoka katika hali yake ya kudhulumiwa.

## 2.2 Muhtasari wa *Nguvu ya Sala*

Mhusika mkuu katika riwaya hii ni mwanamke anayeitwa Susan Ngunze. Yeye ndiye kifungua mimba katika familia ya watoto wane, wote wakiwa wasichana; Roselyn, Jacquiline na Redemta. Babake ni Richard Ngunze na mama yake anaitwa Mary Kasiva.

Susan Ngunze ni msichana mwerevu shuleni na anasoma hadi chuo kikuu cha Nairobi. Kwa vile wazazi wake ni waumini wa Kanisa la AIC, wamesawiriwa kama wafuasi sugu wa imani za Kikristo. Kwa hivyo, Susan analelewa katika msingi huu wa dini. Msingi huu unamwongoza hata kubakia kuwa bikira hadi anapomaliza masomo yake ya chuo kikuu. Kulingana na riwaya hii, huenda Richard anawapa bintize mafunzo makali ya kidini ili wasipitie majaribu aliyoyaona Nairobi alikokuwa akifanya kazi.

Mary na Richard wanakutana Uhuru Park katika mahubiri ya Injili. Baadaye wanafunga ndoa pasipo Richard kugundua kuwa tayari Mary alikuwa mja mzito. Susan anapozaliwa muda mfupi baada ya arusi, ambayo pia inaharakishwa kwa manufaa ya Mary, Richard anamkataa Mary na hata kumpiga kwa kumshuku kuhusu mimba hiyo.

Wakati Susan ni mtiifu kwa wazazi wake kwa kuweka nguvu ya sala mbele ya mambo yake yote, dadake Roselyn anakiuka maadili na kuwa mkaidi. Baadaye

anafukuzwa shule kwa sababu ya kupata mimba. Richard anamfukuza Roselyn na kumfanya akimbilie kwa jirani yao Mzee Nikodemus.

Susan anaporudi nyumbani baada ya kumaliza kozi yake chuoni, anakumbana na hali hii na kumuuliza Richard aliko mnuna wake Roselyn. Swali hili linazua mjadala mkali na mrefu kati ya Susan na wazazi wake. Susan hata anamwambia babake kuwa imani inayovunja familia haifai. Anawafichulia wazazi wao yote kuhusu kosa lao la kuifanya dini kuwakosesha mapenzi kwa watoto wao. Baada ya muda mrefu wa majibizano haya makali, Richard anaridhia na kujitolea kwenda kumrudisha Roselyn kutoka kwa Mzee Nikodemus. Hatua hii inawafanya Mary, Jacquiline na Redemta kumpongeza Susan kwa ushindi wake. Hii ni ishara ya ushindi wa mwanamke dhidi ya uonevu wa kiubabedume.

### 2.3 Mwanamke Kunyanyaswa katika Misingi ya Kidini

Asasi ya dini ndiyo inayotawala riwaya hii tangu mwanzo hadi mwisho. Sheria nyingi za kidini zinatumika kumkandamiza mwanamke. Susan anakatazwa kuwatembelea au kucheza na watoto wasio wa familia za kikristo. Anapopatikana na kosa hili anapigwa sana na babake.

*Alinicharaza kwa mishipi. Nililia na sauti lakini haikusaidia. Aliendelea kunipiga. Wadogo zangu*

*walianza kulia. Vilio vilikuwa vya kupokezana siku hiyo. Mama alishindwa kutusaidia. Aliketi akimwangalia baba aliyekuwa akifoka kwa hasira aliyokuwa nayo.* (uk.3)

Kimya cha Mary kinaashiria kuwa sheria za dini hazijali umri wa mwanamke anaponyanyaswa. Mume ndiye kiongozi wa familia. Mwanamke hana nafasi katika malezi ya watoto. Maongezi kati ya Susan na mamake (uk.2) yanathibitisha hali hii. Hali hii ndiyo chanzo cha maonevu kwa mwanamke.

Ithibati hii inapatikana kwa de Beauvoir (1993: 103-104) asemapo kuwa itikadi ya kikristo imechangia si haba katika unyanyaswaji wa mwanamke. De Beauvoir anaongezea kuwa haiwezi kubadilika kuwa mwanamke anakusudiwa kuishi chini ya uwezo wa mwanamume na hana mamlaka juu ya mume wake. Haifai dini itumike vibaya kumkandamiza mwanamke ambaye anastahili haki sawa na mwanamume katika maisha ya familia na jamii.

Terborg-Penn (1989:xvi) anadhihirisha fikira hii anapodai kuwa wanawake wa kifrika wana nafasi finyu sana katika nyadhifa za kidini sawa na wenzao weusi barani Marekani.

## 2.4 Wanawake na Mavazi Yasiyokubalika katika Dini

Kanuni za kidini hazikubali mwanamke kuwa na sura inayokwenda kinyume na maadili ya kidini. Roselyn, mnuna wake Susan, anapigwa na baba kwa kuvaa ushanga. Hata shuleni wasichana hawakuruhisiwa kuwa na nywele ndefu kama Susan anayekatazwa na babake asifanye hivyo (uk.30). Ni haramu kwa mwanamke kuvaa mapambo kwani ni kinyume cha kaida za kidini.

> *Baba anashikilia kuwa mapambo ya aina hiyo hayakuwa ya kikristo. Alifananishwa na makoa na misewe iliyovaliwa na wacheza ngoma za kienyeji, wakala wa shetani.* (uk 125)

Kwa mujibu wa de Beauvoir, mwanamke anapovaa vizuri ili aheshimike katika jamii, mwanamume anamwona kama pambo na kumtamani kimwili. Imani kama hii ndiyo inamtia Richard hofu juu ya bintiye. Hata hivyo, hatua ya kumpiga Roselyn ni kumnyima mwanamke haki ya kujipamba apendeze na aheshimike. Si kweli kuwa kujipamba ni utovu wa maadili ya kidini. Dini haifai kutumiwa vibaya kumnyima mwanamke uhuru wake wa kujistarehesha. Mawazo kama haya yamepitwa na wakati, na hivyo kuzuia ubainishaji na ukombozi wa mwanamke katika jamii.

## 2.5 Mafundisho ya Lazima ya Dini

Katika nyumba ya Richard, mafundisho ya kidini hayakuwa ya hiari. Richard kama Pasta wa kanisa la AIC la Kiuu, angependa awaonyeshe wazee wa kanisa kuwa anaiongoza familia yake kikristo. Susan anashurutishwa kudurusu "Sala ya Bwana". Anahitajika kuikariri sala hii mbele ya wazee kanisani siku ya Jumapili. Ingekuwa heri kutelekeza kazi ya shule kuliko kuacha kazi aliyopewa na baba. Susan alimwogopa Richard kuliko walimu wake shuleni.

> *Nilihiari kutelekeza kazi ya masomo. Walimu wasingenipiga sana kwa kuitelekeza kazi yao. Lakini baba? Labda angeniua kama ningeshindwa kusoma kwa ghaibu Sala ya Bwana.* (uk.4)

Wakati huo huo, kila jioni Redemta na Jacquiline wanakaa kando ya Richard kwa somo la Biblia. Hawafurahii hali hii na hivyo wanaonekana kujigagamiza kuvisoma vitabu vya dini. Mafunzo ya dini huchangia katika malezi mema ya watoto. Lakini kumlazimisha mtoto wa kike kuwa iwe ndiyo njia ya kumdhibiti, ni kumfanya mfungwa nyumbani kwao. Labda haya yanatokana na ukweli wa madai ya de Beauvoir (1949) kuwa Mtakatifu Paulo aliagiza kuwa upole wa mwanamke ni katika Agano la Kale na Jipya.

Mafundisho yaya haya ya kidini yanampa mwanamke sura ya chanzo cha maasi. Richard anawafunza bintize kuwa Hawa katika Biblia ndiye aliyeshawishika na nyoka na kumwingiza Adamu katika dhambi (uk47). Wazo hili pia linaelezwa na de Beauvoir (1949:104) kuwa mwanamke ndiye mlango kwani Hawa ndiye aliomwongoza Adamu dhambini. Mafundisho haya yanampa mwanamke picha mbaya katika dini. Amesawiriwa kama chanzo cha dhambi duniani. Kwa kufanya hivi, dini inamweka mwanamke kando na kumnyima hata nafasi ya uongozi kanisani. Katika riwaya hii, viongozi wa kanisa ni wanaume.

### 2.6 Wanawake na Kicheko kwa Sauti ya Juu

Akiwa pasta wa kanisa, Richard hataki binti zake wakose maongezi mema ya kikristo. Anampiga Susan kwa kumsikia akicheka kwa sauti ya juu. Mwanamke kama mwanadamu, hana budi kuchangamkia kitu kinachomfurahisha. Kicheko ni njia mojawapo ya kuonyesha furaha. Hatua ya baba kumkataza bintiye asicheke ni ukiukaji wa haki za mwanamke.

> *Baba aliichukia tabia hii ya kuangua kicheko.*
> *Alisema haikuwa tabia nzuri kwa mtoto wa kike.*
> *Nakumbuka jinsi alivyonicharaza siku moja baada*
> *ya kunisikia nikicheka kwa sauti ya juu.* (uk. 33)

Hapa mwandishi anaonyesha jinsi dini inavyomwekea mwanamke vikwazo vikali. Kicheko ni hali ya kibinadamu. Kumkataza mtu kucheka ni sawa na kumnyima haki ya kuwa mwanadamu. Hii ni kumnyima mwanamke haki ya kuishi kwa furaha. Kila kinachokatazwa na dini, kinamlenga mwanamke tu. Dini isitumike vibaya kumnyima mwanamke haki yake kwa sababu tu ya jinsia yake. Millett (1970:99) anayataja mazingira haya "utumwa wa kinyumbani" ambapo mwanamume huwamiliki mke na watoto wake.

## 2.7 Mwanamke na Uhuru wa Kujitumbuiza

Dini ina sheria kuwa mwili wa binadamu, ni hekalu la Bwana. Ni marufuku kuichafua nyumba ya Bwana. Roselyn ana uraibu wa kusikiliza redio na akiwa nyumbani hujitumbuiza kwayo. Lakini anakatazwa na babake kusikiliza redio wala kucheza muziki kwa kunengua kiuno. Richard anamwona bintiye kama mfuasi wa hila za shetani. Anaziita nyimbo za redioni nyimbo za kumtukuza mfalme wa giza (uk.8). Kuchezea mwili ni kuufanya kuwa pango la hila za Lusiferi (uk. 110 -111).

> *Alikuwa akiuchezesha mwili wake kufuatia mapigo ya wimbo huo wa lugha ya Kiingereza. Roselyn alikuwa karibu na dirisha lililoelekea upande wa chini, akinengua kiuno huku akitupa macho ya kuiba huko nje. Alichelea kukutwa seli*

*na babake; ingekuwa kiama kama angetekwa bakunja akiuchezesha mwili wake.* (uk110)

Sheria za dini zinamnyima mwanamke uhuru wa kujitumbuiza. Tabia hii humfanya kuishi na woga na hivyo kukosa nafasi ya kujikomboa. Millett (1969:98) akimnukuu Ruskin anasema, "Ruskin anashauri ajifungie (mwanamke), atosheke na matukio ya kuvutia yaliyothibitishwa na sheria za kidini zilizotolewa zamani. Katika tukio la awali Roselyn anakatisha wimbo kwa hofu ya kupigwa na babake.

*Richard anajikohoza kupitisha ujumbe fulani. Ile sauti ilimfikia Roselyn. Aliukatiza wimbo wake kabla ya kufikia kipokeo chake.* (uk 8)

Hali ya kupigwapigwa Roselyn kila wakati ni ishara ya mwanamke kudhibitiwa kimabavu na kunyimwa nafasi ya kufurahia chochote maishani. Kumfungia mwanamke katika sheria zilizopitwa na wakati ni ithibati kuwa jamii husika haina nafasi ya ubainishaji na ukombozi wa mwanamke wa enzi ya sasa.

## 2.8 Uchungwaji wa Mwanamke

Watoto hutumwa kutekeleza shughuli mbalimbali ndani na nje ya nyumbani kwao. Richard amewawekea bintize sheria kali ya kutokawia wakitumwa nje. Anamwuliza Susan sababu ya akina Jacquiline kukawia kutoka sokoni walikotumwa (uk.105). Sheria hii inaonyesha jinsi kanuni za dini zinatumika vibaya kumtawisha mwanamke asibanduke kutoka nyumbani. Susan anathibitisha haya anapodai kuwa hajawahi kuingia mjini ila tu alipopelekwa hospitalini (uk.30). Hizi ni sheria kali za kumdhibiti mwanamke asiwe na uhuru wa kujumuika na majirani. Kwa mujibu wa Millett (1969:99), watumwa wengi wana haki nyingi zaidi ya wanawake walio chini ya sheria. Utumwa wa jinsi hii ni moja kati ya pingamizi nyingi dhidi ya ukombozi wa mwanamke. Dini haifai kutumika vibaya kumkandamiza mwanamke kwa njia yoyote ile.

Kupitia Susan, tunafahamishwa sehemu kubwa ya mafundisho ya mamake kumtahadharisha dhidi ya kupatikana kwenye kundi la wavulana, hasa Susan anapojiunga na shule ya sekondari na baadaye chuo kikuu. Richard alishindwa kuvumilia hali hii.

> *"Aliwasindikiza nani?" aliuliza baba baada ya kimya.*
>
> *"Tulisindikizwa na James." Nilijibu.*
>
> *"Eh....Eh huyo ndiye rafiki yako eh!* (uk. 106)

Mafundisho kama haya yamenata akilini mwa Susan. Cedric anapomwalika Susan katika dhifa ya kusherehekea siku yake ya kuzaliwa, Susan anaandamana na rafiki zake wa kike, June na Catherine, asije akaingia mtego wa mwanamume (uk.169). Kwa mtazamo huo huo Susan anachelea kuingia kwao kutoka shuleni baada ya masomo ya sekondari akiandamana na Cedric. Anapoulizwa alivyobeba mizigo yake, anajibu kuwa haikuwa mizito sana (uk.128).

Ni jambo la busara kuhakikisha watoto wa kike wamelelewa kwa uadilifu. Lakini hiki kisiwe kisingizio cha kumfanya mtumwa. Nia ya Richard na Mary kuwaadilisha binti zao ni jambo la kusifika ila tu isiwe njia ya kuwanyima haki zao. Kumfanya Redemta kuwa mchungaji wa Susan njiani, ni kuvunja haki ya mtoto wa kike. Msichana kupatika katika kundi la wavulana wenye nia njema si jambo la kutiliwa shaka. Hii ndiyo sababu ubainishaji na ukombozi wa mwanamke unafaa upewe kipaumbele ili kuondoa vizingiti kama hivi vinavyomkandamiza msichana.

**2.9 Mwanamume kama Kiongozi wa Dini**

Kazi nyingi za fasihi na mahubiri ya viongozi wa kidini humkengeusha na kumdhalilisha mwanamke (SIDA2009:22). Madai ya Terborg-Penn (1989:xvi) yanathibitisha kuwa, wanawake wa Afrika wana nafasi finyu katika

nyadhifa za kidini. Shughuli zote za dini zinaongozwa na mwanamume. Isipokuwa mwanzoni, Mary akimsaidia mumewe Richard, hakuna popote tena katika riwaya hii tunapomwona mwanamke akiwa na jukumu lolote kanisani. Wanaume ndio wanawajibishwa kama vile Richard, Nikodemus na Deo Mukusya. Deo na Nikodemus wanapewa jukumu hili licha ya wao kuwa walimu wakuu katika shule za msingi kijijini kwao hali ambayo ingewapokonya nafasi ya kutosha kulitumikia kanisa. Richard anapewa uongozi wa kanisa baada ya pasta wa zamani kustaafu.

> *Haukupita muda mrefu. Wazee wa baraza la kanisa walimteua Richard Ngunze kuwa msaidizi wa Deo Mukusya.* (uk 178)

Mary na mkewe Nikodemus walibakia wake wa nyumbani licha ya kuwa wote walikuwa wafuasi sugu wa dini yao. Dini inamtawisha mwanamke akishughulikia kazi za nyumbani wiki nzima. Huenda huu ndio mtazamo unaorejelewa na Morgan (1992:76) kuwa karne tano za desturi za ukristo na uislamu zilichangia kudai kuwa wanawake ni wachafu na najisi. Madai kama haya yanawachafulia wanawake sifa na hivyo kuwazuia kupata ubainishaji na ukombozi ambao wameupigania kwa karne nyingi sasa.

## 2.10 Mwanamke Kubaguliwa Kitamaduni

Kubaguliwa kwa mwanamke katika msingi wa mila na desturi ni mtazamo unaompunguzia thamani katika jamii anamoishi. Mambo yanayoleta maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kitamaduni huegemea upande wa kiume. Mwanamke anahusishwa na imani hasi zinazochangia kuivunja au kuigonganisha jamii. Kwa mfano, Richard hampi mkewe Mary hata nafasi ya kueleza kumhusu Susan kwani ndiye kiini cha dhiki za Richard dhidi ya wanawe kupitia shaka la mimba yake ya kwanza.

Mwanamke anachukuliwa kama ishara ya mikosi na majanga ya kijamii. Cha kushangaza ni kuwa, imani kama hizi za kibaguzi zinakuzwa na kuendelezwa na wanawake wenyewe. Mhusika Nzisa, mamake Richard, anapoelekea mlima wa Kititu kumtafutia Richard matibabu ya kienyeji, anaomba asikutane na mwanamke njiani (uk.35). Syokulu, mganga mwanamke, pia anaamini kuwa kazi yake ingekuwa nzuri iwapo mteja wake wa kwanza angekuwa mwanamume. Kuna imani kuwa wanawake wana kisirani. Syokulu alifunzwa imani hizi na mamake ambaye ndiye aliyemwachia mkoba wa uganga.

Hizi ndizo itikadi potofu ambazo Moi akimnukuu Millett (1969) anasema kuwa ni sharti mwanamke azitambue na kuzitupilia mbali ili awe huru kwani ni za kiubabedume wa wananume ili waendelee kumdhibiti kiakili (Moi 2002:29).

Mary anaaguliwa na Syokulu kuwa ugonjwa wa Richard unatokana na kurogwa na mamake Stephanus. Maelezo ya Syokulu ni kuwa mamake Stephanus alifanya hivyo ili kulipiza kisasi kifo cha bintiye kinachoaminika kilitokana na uchawi wa Nzisa. Mambo ya ushirikina hapa yanamzunguka mwanamke tu huku mwanamume hashirikishwi nayo. Msimamo huu wa jamii unaharibu sifa za mwanamke kwa kumbagua kama njia ya kupinga ukombozi wake. De Beauvoir anadai kuwa mambo ya kutisha yanasukumiwa na mwanamke kwa mwanamume kwa sababu ya jinsia yake.

## 2.11 Mwanamke kama Chombo cha Kufukuzia Mikosi ya Kijamii

Bundi ni mmoja kati ya ndege wanaohusishwa na mikosi na majanga yanayoikumba jamii ya binadamu. Sauti yake ikisikika karibu na makazi inafasiriwa kuwa lazima patokee msiba. Mary anaposikia sauti ya bundi karibu na zizi la ng'ombe anamtupia kijinga cha moto. Susan naye anatiwa hofu na sauti hiyo hiyo akielekea jikoni (uk.12). Tunamwona Nzisa anapoelekea kwa Syokulu kule mlimani Katitu akijaribu kudadavua sauti ya bundi kati ya ndege wengine isije ikamtilia safari yake nuksi. Anafurahi sana kwa kutosikia sauti ya ndege huyo (uk 35).

Ithibati ya kuchukiwa kwa ndege huyu inaonekana siku ya kifo cha Mzee Nzimba, babake Richard, Nzisa anaposumbuliwa na sauti ya bundi.

> *Alipomaliza shughuli yake, alianza kuelekea ilipokuwa nyumba alimokuwa mumewe. Viwambo vya masikio yake vilinasa mawimbi fulani ya sauti. Alisimama kwa muda wakati akili yake ikiwa katika harakati za kuipambanua sauti hiyo. Aliyatega masikio yake imara na mara hii haikurudi mufilisi ila yalifanikiwa. Ilikuwa sauti ya bundi.... Watu walisema kuwa kila aliapo ndege huyo karibu na makazi ya watu pangetokea dhara kubwa hasa kama alikuwepo mgonjwa katika mji uliohusika.* (uk.52 -53)

Nzisa kwa hofu kubwa, aliishiwa nguvu ya kumfukuza ndege huyo. Wakati huo huo ndipo roho ya Mzee Nzimba ilipomtoka. Jazanda ya bundi kuhusishwa na wanawake ni ishara kuwa jamii inamchukulia mwanamke kama kiumbe anayehusishwa na nuksi na mikosi katika jamii. Imani kama hizi zinamfanya mwanamke aonekane kama mja aliyelaaniwa na hivyo kumzuia asipiganie haki yake. Jamii inafaa iuache mtazamo huu wa kijadi unaomfungia mwanamke njia za kujikomboa. Huu ndio ujumbe anaupigia upatu mtunzi wa riwaya hii kuwa mawazo yaliyopitwa na wakati yasiwakoseshe wanawake

ukombozi wao. Hii si karne ya wanawake kufikiriwa kama viumbe wachafu na najisi kulingana na wazo la Morgan (1992).

## 2.12 Mwanamke Kutengwa na Malezi ya Watoto

Mara nyingi katika familia ya Richard, ni yeye ndiye tunayemwona akishughulika na malezi ya watoto. Kila mara hamhusishi Mary anayebakia mtulivu Richard akitekeleza mambo ya malezi kwa binti zake. Maongezi yake Susan na mamake (uk.2) na hatua zilizochukuliwa na Richard (uk.3) ni ushahidi ulio wazi. Richard anapompiga na kumburura Susan hatumwoni mamake akiteta kwa udhalimu huu dhidi ya bintiye.

> *Mama alishindwa kutusaidia. Aliketi akimwangalia baba aliyekuwa akifokafoka kwa hasira aliyokuwa nayo.* (uk.3)

Ukatili wa Richard kwa bintize unailaza njaa familia nzima. Hii ni ishara kuwa jamii inamdhalilisha mwanamke anayeonekana dhaifu hata mbele ya wanawe. Millett (1969:67) anatujulisha mamlaka ya mwanamume juu ya mwanamke kuwa kama mkuu wa familia, mume alikuwa mmilikaji wa pekee wa mke na watoto. Mtazamo huu wa jamii unamfanya mwanamke awe sehemu ya mali ya mume kwa hivyo hana sauti juu ya chochote katika mji (SIDA2009:67). Hali hii inamdhulumu mwanamke na hiyo ndiyo babu ya kuwepo haja ya kumpa

utambulisho ili ajikomboe. Kongamano la Mwongo wa Wanawake wa Umoja wa Mataifa lililofanyika Nairobi (1985), lilipendekeza kusaidiwa kwa wanawake wanaopitia mateso kama kupigwa, viungo vya miili yao kuharibiwa, kuchomwa, kunyanyaswa kimapenzi na kubakwa (Turshen na Holcomb:1993;103). Wanaongezea kwamba ukatili dhidi ya mwanamke ni kwa njia ya kuudhibiti uwezo wake wa kila sehemu ya maisha kuanzia nyumbani hadi shuleni, mahali pa kazi na sehemu nyingi za umma. Katika makongamano kama haya kuhusu dhuluma dhidi ya mwanamke ulimwenguni, kuna mapendekezo kama kubadili tabia ili kuzuiwa ama kupunguzwa kwa ukatili huu. Kuna athari za kisaikolojia kwa wanawake kupitia mateso katika jamii zinazotawaliwa na wanaume (Eagleton 2007:159).

Kutoshirikishwa mwanamke katika maamuzi ya nyumbani kunadhihirika pale Richard anapokataa ushauri wa mkewe Mary kuwa asikate mti wa mkuyu alivyokatazwa na mzee mmoja kutougusa kwa kuwa ni madhabihu. Hisia zinazomfanya Richard apuuze ushauri wa mkewe ni mgongano kati ya imani ya kidini na kitamaduni. Aliamua aukate ule mti na mara nyoka alitokea na alipomwona nyoka, Richard alitoroka hadi nyumbani.

> *Richard Ngunze alijitia mwapuza, asingemsikia mkewe. Alikumbuka jinsi wanawake walivyokuwa*

*chanzo cha maasi. Walikuwa vishawishi vya uovu; adhabu isiyoweza kukwepeka.* (uk.7)

Kinachosikitisha ni kuwa ukatili kwa mwanamke unahusishwa na muundo wa kiubabedume ulioratibishwa na familia za kiume zinazounda asasi zinazomfanya mwanamke kuwa chini ya mwanamume na mamlaka zake (Turshen na Holcomb 1993:89).

## 2.13 Mwanamke na Suala la Uzazi

De Beauvoir (1949:71) anadai kuwa watu wa asili hawakufahamu nafasi ya baba katika kumzaa mtoto. Wazo hili lingalipo na wanaume wa enzi hizi. Kwa sababu hii, mwanamke asipozaa au akikosa kumzaa mtoto wa kiume, huchukuliwa ni kosa lake kwa hivyo anaweza kupewa talaka na mumewe.

Panafaa pawekwe mikakati ya mazingira mema ya kuwalinda wanawake kwa kuheshimu uhuru wao kwa kuwapa nafasi ya kuzaa kwa njia inayowafaa zaidi (SIDA2009:80).

Kuna madai kuwa Sista Emilly alitalikiwa na mumewe kwa kukosa kuzaa baada ya kuishi naye kwa muda wa miaka sita. Baadaye, mumewe anamwoa mwanafunzi (uk.63). Richard naye anampiga Mary kwa kujifungua mtoto wa kike. Matumaini yake yalikuwa kumpata mtoto wa kiume. Shauku kubwa ya

wanaume juu ya mtoto akiwa bado tumboni mwa mkewe isiwe kibali cha kuleta usumbufu wa kumtawala mkewe (SIDA2009:75).

Ukatili wa mwanamume kwa mwanamke haujali kuwa uwezo wa kumzaa mvulana au msichana haupo kwenye uwezo wa mwanamke. Uzazi wa mwanamke katika ulimwengu mzima hutawaliwa na mume wake, familia na jamii kwa ujumla (SIDA2009:72).

Kupigwa huku kwa Mary huenda kulikuwa na sababu mbili. Kwanza, shaka juu ya mimba kutokuwa ya Richard na pili, kutotimiza matarajio ya kumzaa mvulana.

> *Lakini huu mwezi wa saba tu. Inawezekana mtu anajifungua hata baada ya miezi saba.*
>
> *Ni vigumu.*
>
> *Si ajabu. Hasa kwa mtu anayejifungua kwa mara ya kwanza.*
>
> *Mm…….. sidhani.*
>
> *Labda hiyo mimba siyo yako!*
>
> *Haiwezekani!* (uk 179)

Kosa lingine la uzazi linampata Roselyn anapopata uja uzito akiwa shuleni. Richard anampiga na kumfukuza hata bila ya kujali kuchunguza ni mwanamume gani aliyehusika na mimba hiyo. Susan anaposema kuwa makosa yamo katika malezi Richard aliwapatia binti zake, baba anapandwa na hasira.

> *Siwezi kuvunjiwa adabu na mtoto wangu kisha mtoto huyo awe wa kike.* (uk 196)

Maneno haya makali ya Richard ni ithibati kuwa mwanamume wa Kiafrika anamchukulia mkewe kama chombo tu cha kuzalishia watoto na kutumikishwa nyumbani kwa maslahi ya kiume. Richard pia ni kielelezo cha unafiki katika dini unaomfanya mwanamke kuwa ishara ya maovu yote katika jamii. Utata uliopo kwenye kauli hii unafanya iwe vigumu kujua kama mkosa adabu ni Roselyn kwa kupata mimba, au ni Susan kwa kumkosoa babake. Mwanamke anapokosa, suluhisho huwa ni kumwadhibu kwa kipigo kumfukuza na kumtenganisha na familia yake. Bora zaidi, suluhu la tatizo litokane na kutambua kiini cha tatizo lenyewe. Hapa tatizo lenyewe ni malezi waliopewa watoto hawa na wazazi wao, Richard na Mary. Turshen na Holcomb (1993:89) wanasema kuwa wanawake hutengwa na waume zao kufuatia wivu dhidi yao huku wanawake pia wakijitenga wenyewe kwa sababu za hofu za kufedheheshwa kwa muda wa miezi kadha. Mwanamke

akijikomboa, atapata uwezo zaidi wa kupigania maovu kama haya dhidi yake na kuyatokomeza.

### 2.14 Mwanamke Kudhibitiwa Kimabavu

Jamii ya riwaya hii inaonekana kuwa na imani kuwa nguvu na ukali ni sifa iliyotengewa mwanamume pekee. Hali hii inadhihirisha ukatili wa kumpiga mwanamke kila anapodhaniwa kuwa ana kosa. Mwandishi anamsawiri Richard kama mhusika katili kwa wanawe na mkewe. Susan anapigwa kwa kwenda kucheza na watoto wasio wa familia ya kikristo. Roselyn naye anapigwa kwa kuvaa ushanga na kupata uja uzito. Mary anapigwa kwa kujifungua mwana wa kwanza wa kike huku Mwalimu Bonifas Ngewa akidaiwa kumpiga mkewe kila jioni (uk.15).

Sokoni, wasukuma rukwama wanamgonga mwanamke aliyesimama njiani licha ya watu kama hawa kutazamwa kuwa duni kijamii. Isitoshe, wanawake wawili wanapokonywa vibeti vyao jijini Nairobi. Vijana waliokosa ajira na kugeuka kuwaibia wanawake wakishikwa, matusi ni upande wa mwanamke. Mwizi aliyeshikwa anapigwa na kutukanwa kuwa ana sura kama ya nyanya yake (uk 115).

Nguvu nyingi kupita kiasi hutumiwa kumrekebisha mwanamke anapokosa. Mara nyingi kwa kweli, si kosa ila ni maonevu tu. Richard kama tulivyotaja

hapo juu, anawapiga binti zake kwa kisingizio cha kuwapa malezi ya kimaadili. Hajali hata kama kipigo kinamwumiza mtoto.

*Susan mbona uso wako umevimba hivi?*

*Nilipigwa jana jioni.*

*Na nani?*

*Baba.*

*Kwa sababu gani?*

*Nilicheza na watoto wa jirani.*

*Hilo tu?* (uk 4).

Kauli hii inatokana na maongezi kati ya mwalimu na Susan baada ya kupigwa na babake jioni ya siku iliyitangulia. Shuleni mambo ni yale yale. Dora anafuraha ya kumaliza masomo ya shule ya msingi. Anapoulizwa sababu, anamweleza Susan wazi maoni yake.

*Maisha ya shule ya msingi yana matatizo sana;*

*kosa dogo tu viboko.* (uk 18)

Mwalimu Bonifas Ngewa anaogopwa na wasichana kwa kuwachapa wakishindwa kumudu somo la hisabati.

Moi anaelekea kuguswa na hisia kama hizi anapomnukuu Millett kuwa utawala wa kijinsia ndio itikadi za kitamaduni za mwanamume na matarajio yake kumfanya mwanamke kubakia chini yake (Moi2002:26).

Suala la kumwonea mwanamke kwa kuchukuliwa kuwa mnyonge asiye na nguvu dhidi ya mwanamume si jambo la ustaarabu. Lililo la busara ni kumpatia mwanamke utambulisho na kupewa ukombozi awe na haki sawa na jinsia ya kiume. Tabia ya kupigapiga wanawake haifai kuendelezwa kwani imepitwa na wakati.

Millett kwa kuwahurumia wanawake anatoa hoja kuwa wanawake kiasili ni watiifu na wanaume ni watawala na wenye nguvu hivyo, hujiona ndio wenye haki ya kuwatumikisha kwana kwamba wanawake hufurahia na kustahili udhalimu (Millett1969:203).

**2.15 Mwanamke kama Chombo cha Burudani**

Mwanamke huchukuliwa kama chombo cha kutoshelezea ashiki ya mwanamume. Katika riwaya hii mwandishi anaelekea kukosoa mazoea ya walimu kuacha majukumu ya ulezi na kuwageukia wanafunzi wao wa kike kimapenzi.

Mwalimu Octavian Birundu anatabia ya kuwatongoza wasichana wa shule na hasa wanaojiunga na kundi linaloongozwa naye la uigizaji. Akiwa ndiye

mshauri wa wanafunzi (wasichana), Birundu anatumia nafasi hii kuwashawishi wasichana kumtimizia haja yake ya kimwili. Mwalimu Birundu anamtuma Bethsheba amwite Susan aende nyumbani kwake. Rose anapewa pesa kama kishawishi cha kumpata Susan. Isitoshe, Rose anapewa nakala ya mtihani wa hisabati.

> *Kwani unafikiri huu mchezo? Nimepata mia mbili za lunch.*
>
> *Mm ... ... .... Naona umewahi.*
>
> *Tena sana ... ... ... ... basi unajua nini?*
>
> *Amenipa copy ya karatasi ya Hisabati.*
>
> *Ile ya kesho?* (uk 94)

Deogratias Manyara, tajiri mmoja Kileleshwa Nairobi na mwajiri wa Mary, anamdhulumu Mary kimapenzi na kumtungisha mimba mara mbili (uk 166). Ili kuitia doa tabia hii, mwandishi anatueleza kuwa Birundu hatimaye anaachishwa kazi ya ualimu kwa kumtungisha mmwanafunzi wake mimba. Tabia kama hii inawanyima wasichana nafasi ya kujiendeleza kielimu na katika hali hiyo kukosa nafasi ya kujikomboa kutoka kwenye manyanyaso ya mwanamume.

## 2.16 Suala la Urithi Katika Jamii

Kaida za kitamaduni zinambagua mwanamke na suala la urithi. Nafasi hii amepewa mwanamume pekee. Mume akifa kabla ya kugawa mali yake kwa wakeze, mwanamke anazongwa na matatizo ya kuzozania mali na jamaa za marehemu. Wake zake Mzee Nzimba wanajikuta mashakani mume wao anapokufa kabla ya kuigawa mali yake.

> *Mzee Nzimba mwenyewe alifanya kosa kwa kutoigawa mali yake kabla ya kifo chake ..... jamii iliamini kuwa hivyo ndivyo ilivyotakiwa kwa mtu aliyekuwa na jamaa kubwa* (uk 71).

SIDA inagusia suala hili kwa uchungu inaposema kuwa, haki ya urithi na ile ya mjane ukiwemo ubabe wa wanaume, ni masuala yanayowakumba wanawake wa matabaka yote na hivyo kuibua mchakato wa umoja wa wanawake katika kudai haki zao (SIDA 2009:18).

Jamii inamkandamiza mwanamke na kumnyima haki ya kumiliki mali. Hali hii inamfanya mwanamke kukosa uwezo wa kiuchumi. Hiki ndicho chanzo cha umaskini wa kumfanya mke amtegemee mumewe daima. Kulingana na Millett (1969:67), mume akifa bila kuacha wasia, serikali inachukua mali yake na kumwacha mjane bila cho chote.

Mwanamke hana mamlaka juu ya rasilimali kwani mwanamume ndiye peke yake mwenye haki katika umilikaji wa mali (SIDA2009:63). Mtazamo huu ni kumnyanyasa mwanake kwani ni sharti mwanamke apewe uwezo wa kumiliki mali ili ajitegemee kiuchumi. Mwanamke akijitegemea kiuchumi, kijamii na kitamaduni atapata nguvu ya kujikomboa kutokana na silisila au minyororo ya kiubabedume. Wanawake hawana budi kuwa na haki na madaraka juu ya rasilimali yao wenyewe inayotegemeka ili kujimudu maishani (SIDA2009:17).

## 2.17 Mwanamke Kudharauliwa na Kutukanwa

Jamii ya riwaya hii inaonyesha dharau iliyokithiri kwa mwanamke hata bila kujali umri wake. Dora anachokozwa akiwa kati ya watoto wenzake wavulana wanapotoka shuleni. Anafanyiwa stihizai kwa kuwa na kovu kwenye shavu lake la kushoto. Anachukizwa sana na tabia hii na hata analia. Bethsheba naye anaitwa twiga kwa msingi wa miguu yake mirefu. Kebehi hizi zinatokana na hatua zake ndefu anapokimbia. Steve Malelu ndiye chanzo cha kuitwa jina hili. Anapoulizwa na mwalimu sababu ya kuwa mwisho kuzunguka uwanja, anatoa kisingizio.

> *"Mbona ukawa wa mwisho?"*
>
> *"Mwalimu hatua zangu ni fupi sio kama za twiga," alisema Steve huku bado akihema.*

*Darasa zima liliangua kicheko.... Tangu siku hiyo Bethsheba alipachikwa lakabu ya twiga.* (uk 16).

Richard anamtukana bintiye Roselyn kuwa kiruka njia na mwana harashi anapogundua kuwa ni mjamzito. Kitendo cha kumfedhehesha mwanamke kinafaa kutupiliwa mbali kwani badala yake mwanamke anahitaji kutambuliwa kama binadamu anayestahili haki na heshima.

## 2.18 Majukumu Mengi ya Mwanamke katika Jamii

Mwanamke ana majukumu mengi kupindukia katika jamii inayopatikana katika riwaya hii. Mwanamke anatakika kumheshimu mumewe, kutekeleza majukumu ya nyumbani, kuteka maji, kutafuta kuni na kazi za sulubu za shambani bila kutaja kuwajibikia uzazi na ulezi (SIDA 2009:87).

Mwanamke ana shughuli za kutekeleza mchana na usiku. Mwanamke ni mpishi, mlezi, mzazi, mke, mganga na hivyo hana nafasi ya kujipumzisha. Mbali na kazi ya shamba na upishi, mwanamke ndiye anayemtunza mumewe na watoto wake. Nzisa anamtafutia Richard matibabu kwa Syokulu kule mlimani Katitu. Bintize Richard ndio wanaowapeleka ng'ombe malishoni huku yeye akibaki nyumbani huku kushinda akisoma Biblia.

Kuna majukumu ya kishirikina. Mary anamrushia bundi kijinga cha moto usiku anaposikia sauti yake karibu na zizi la ng'ombe. Wanuna wake Susan wanaokota kuni chini ya mti wa mkuyu (uk.20). Wanawake watatu wanauza uji mjini Machakos ili kuwakimu jamaa zao. Mary anatoka kijijini kwao na kufanya kazi ya uyaya katika mtaa wa Kileleshwa Nairobi. Mke wake Nikodemus anazaa bila kupanga uzazi na hivyo kubebeshwa mzigo mkubwa. De Beauvoir (1949:108) anataja hali hii ya umama kuwa zaidi ya utumishi kuliko kuwa mshirika.

Kwa vile mwanadamu anahitaji kujipumzisha ili apate nguvu na afya, majukumu ya mwanamke yanamfanya mtumwa wa mumewe. Mwanamume ni sharti amsaidie mkewe kazi ili isiwe kuwa mwanamke anakosa nafasi ya kujistarehesha. Hii ndiyo hali inayofanya kuwepo na umuhimu wa upiganiaji wa haki ya mwanamke ili afikie ukombozi wake.

## 2.19 Jitihada za Kumbainisha na Kumkomboa Mwanamke

Mwanamke anastahili aopolewe kutoka kwenye lindi la dhuluma na manyanyaso ya jamii. Ukombozi wake hauwezi kufaulu iwapo hapatakuwapo na ushirikiano wa jinsia zote mbili. Mwandishi amejitahidi sana kumwinua mwanamke kwa kupitia elimu katika riwaya hii. Wanawake wengi waliotajwa humu, wana kiwango fulani cha elimu. Susan, Catherine na June wamefikia

kiwango cha chuo kikuu huku Bethsheba na Roselyn kufikia elimu ya sekondari.

Watoto wa Richard wote wane, pamoja na msimulizi wa hadithi hii kuwa wasichana, ni hatua nzuri ya kumwinua mwanamke. Kuwepo kwa mwanamke kuwa ndiye mhusika mkuu, kunatoa nafasi ya kumwendeleza hadi kufikia upeo wa kujiendeleza na kujikomboa. Ni jambo la kutia moyo kuwa baada ya kupata elimu wa chuo kikuu Susan anapata ujasiri wa kumkabili babake aliyetumia vibaya dini kuwapatia malezi ambayo hayakumfaa Roselyn maishani.

### 2.19.1 Mwanamke Kupata Elimu ya Kutosha

Susan ni mhusika mwenye bidii shuleni akiwa pamoja na wenzake Catherine Ouko na June. Kwa akili nzuri waliokuwa nayo, wamejibiidisha hadi chuo kikuu na kusomea taaluma mbalimbali. June anasomea taaluma ya biashara, Catherine Ouko, udaktari na Susan akisomea fasihi katika Kitivo cha Sanaa. (uk 137).

Kwa vile ukombozi wa mwanamke unahitaji utaalamu wa hali ya juu, Susan anaazimia kusoma kitabu cha mwananadharia wa Virginia, Woolf, *A Room of One's Own,* kinachoshughulikia harakati za ukombozi wa mwanamke (uk 126). Makabiliano kati yake na babake juu ya kufukuzwa kwa Roselyn huenda

yalichochewa na maarifa aliyoyapata kutoka katika mawazo ya Woolf. Katika riwaya ya *The River Between* ya Ngugi wa Thiong'o, Susan anapendezwa na kisa cha msichana aitwaye Muthoni ishara kuwa anavutiwa sana na matatizo yanayomzonga mwanamke. *Miguel Street* ni riwaya nyingine ambayo visa vyake kuwahusu wanawake vinaathiri mawazo ya Susan kuhusu dhuluma dhidi ya mwanamke. Suala la George kuwanyanyasa bintiye Doly na mkewe halimfurahishi. George anampiga mkewe kipigo kinachomsababishia kifo. Mfano mwingine ni wa Laura, mwanamke aliyewazaa watoto saba, kila mmoja na baba tofauti.

Katika kuzisoma riwaya hizi, ni dhahiri kuwa Susan anagundua kuwa katika jamii za ulimwengu mzima, mwanamke ni kiumbe anayedharauliwa na kudhibitiwa kimabavu. Kwa kiasi fulani, huenda vitabu vya fasihi alivyovisoma Susan vilichangia sana mabadiliko ya kimapinduzi aliyoonyesha alipomkabili Richard juu ya imani yake katika dini zilizomkosesha mapenzi kwa wanawe.

Ramazanoglu et al (2002:37-38) wanazungumzia elimu wakisema kuwa, wazo la ukombozi wa wanawake wa miaka ya sabini kwa ujumla lilikuwa la ufuasi wa elimu wa ubinadamu kuwachukulia wanawake kama watawaliwa razini ili kuwawezesha wanawake kuwa na elimu ya kustowafanya watumishi na hivyo kuwakomboa wanawake kutoka katika ukandamizwaji wa kiume. Elimu kwa

hivyo, ndiyo nyenzo inayofaa kutegemewa na wanawake kutimizia harakati za ubainishaji na ukombozi wa mwanamke.

### 2.19.2 Kumwamini Mungu Katika Mambo Yote

Mafunzo ya dini kwa kiasi kikubwa yamechangia tabia njema ya Susan. Susan alikuwa akisali kila alipopatwa na tatizo la kibinafsi. Tunamwona akisali siku ya hedhi yake ya kwanza bwenini.

> *Bwana naomba unielekeze ipasavyo. Naomba usinitie katika vishawishi. Nipe nguvu za kukabili na kushinda hila za maovu. Nielekeze jinsi ya kutunza kanisa lako bwana. Kwa jina la Kristo naomba.* (uk.61)

Kauli hii ni ithibati kuwa Susan alikuwa na imani ya dhati ya dini na hakuwa na shaka na matumizi yake mazuri. "Nguvu ya sala" ilimfanya Susan asitafute ushauri wa mwalimu Octavian ambaye angemwangusha kwa vishawishi vyake viovu (uk 67). Susan pia amehifadhi ubikira wake na hadi mwisho wa riwaya, hatumwoni akiangukia vishawishi vya mapenzi ya mwanamume yeyote. Makabiliano yake na Richard yasichukuliwe kuwa ni kwenda kinyume na mafundisho ya dini ila anamkosoa babake juu ya matumizi mabaya ya dini.

Hata hivyo, Susan hakusita kuyatilia shaka baadhi ya mafunzo ya dini ambazo ndizo zaelekea kuwa chanzo cha kumdhalilisha mwanamke katika jamii. Mary anapomlalamikia aliporudi nyumbani kwa likizo kuwa Susan ameanza kuzembea kazi ya Bwana, Susan anakiri kuona mabadiliko ya ajabu.

> ... ... *Nilishaanza kuyadadisi mambo fulani kuhusu dini. Kwa kwelli siku mama aliponilalamikia nilitaka kumweleza kuwa nilishaanza kuwa na wasiwasi makubwa tarafu ya msimamo wa dini kumhusu mwanamke.* (uk 61).

Sylvester (1994:24) anazungumzia jitihada za matabaka ya wanawake kukataa desturi za dini zinazowawekea mipaka. Kwa hivyo ni dhahiri kuwa matumizi mazuri ya dini yanaweza kuongoza maisha ya binadamu na hasa mwanamke hadi afikie upeo wa kumkomboa kutokana na dhuluma za mwanamume. Hata hivyo, ni jambo la kusikitisha kuwa mafundisho mengine ya dini yamtumia mwanamke kwa njia ya kumfanya aendelee kunyanyasika. Dini nyingi zinamkebehi mwanamke kuwa Mungu atamfidia kwa kuvumilia maisha ya dhiki na taabu yaliyompagaza kwa heshima aliyompa mumewe na nasaba zake (SIDA2009:97). Haya ndiyo madai yanayofanya mwanamke aendelee kunyanyasika chini ya ubabe wa mwanamume na kumnyima nafasi ya kujipatia ukombozi wake.

### 2.19.3 Mwanamke Kupinga Misimamo Mikali

Kuna jinsi ambavyo jamii inayoongozwa na taasubi za kiume kupitia kanuni za dini zinazomwonea mwanamke. Kwa hiyo ni vyema iwapo mwanamke atasimama kidete kuzipinga kanuni hizo.

Roselyn anapokuwa mkubwa, anabadilika na kuwa mkakamavu na kuyapinga mambo yanayoelekea kumnyima haki zake. Anapoulizwa na mamake sababu za kulala nje, majibu yake yanaonyesha kuwa amechukizwa na kuwekewa mipaka kila wakati.

> *Siku hizi mambo yamebadilika mama….*
>
> *Huu ni wakati tofauti… …*
>
> *Ya nini kumweleza na hatakubali? Mtu akinyimwa*
>
> *uhuru hujitwalia.* (uk 187)

Kauli hii inatokana na kuwa Mary anamshauri Roselyn kupata idhini ya babake kila anapotaka kuondoka nyumbani. Mary anasema kuwa tabia ya kulala nje siyo tu kuwa inapingwa na Richard, bali pia hata kitamaduni haikubaliki. Madai haya ndiyo yanayomchochea Susan na kumpasulia Mary mbarika.

> *Utamaduni huo huo ndio unaowafanya wanawake wasipende kujiendeleza, unawadharau na kuwadunisha. Mama wakati tulio nao ni tofauti kabisa na wakati wenu na lazima tuwe na tabia ya kuyachuja mambo yote. Hatuwezi kufuata kila kitu tu kumpendeza baba au kutomwaibisha* (uk 187).

Ujasiri na ukakamavu kama huu ni hatua inayofaa katika kukataa misimamo yote inayomkandamiza mwanamke. Mary anaona mwangaza na hata Richard anaporudi hamwelezi yaliyotokea. Hata hivyo Susan hakumficha babake yaliyokuwa moyoni mwake kuhusu msimamo mbaya wa dini anapotaka aambiwe sababu za kumfukuza Roselyn.

> *Baba naona hata mimi utanifukuza pia. Lakini lazima niseme kuwa dini haipaswi kuwafanya watu wakose mapenzi ya wana wao. Mtu hawezi kumtupa mwanawe kwa sababu ya imani tu; mwanzo hata siku hizi watu hawana imani kubwa na hiyo dini.* (uk 198)

Susan na Roselyn wanaungana na kumwambia Mary kuwa wakati wa kufuata dini na utamaduni bila ya kuchuja umepita (uk. 87). Susan anaonekana

kuchoshwa na ukatili wa babake juu ya hatua ile ile ya kumfukuza Roselyn kutoka nyumbani kwao.

> *Kama kuna makosa yo yote yamo katika malezi mliyotupa. Mmekazania tufuate mafundisho ya Biblia bila ya kutuelekeza katika maisha halisi ya ulimwengu huu.* (uk. 196).

Mawazo ya Susan yalimgusa sana Richard aliyegundua kuwa bintiye hakuwa anatania ila alitaka naye atafakari zaidi. Inafikia hatua ya Susan kuikejeli nguvu ya sala jambo ambalo lilimfanya Richard kuamua kwenda mwenyewe kwa Nikodemus kumrudisha Roselyn nyumbani.

> *Mbona mlimfukuza Roselyn; hiyo nguvu ya sala mliisahau nyie?* (uk 197)

Sylvester (1994:24) anaonyesha jinsi wanawake waingereza walipochoshwa na msimamo mkali wa dini ya Katoliki juu ya wanawake, walizidisha nguvu za kibinafsi kwa kubadili dini kujiunga na Uprotestanti iliyokubali wanawake wa kikabila kuchukua sehemu ya mwamko mpya.

Hatua ya kuipinga misimamo mikali ya dini na utamaduni inapogeuza wazo la Richard, tunawaona Mary, Jacquiline na Redemta wakiungana na Susan kwa kumpongeza kwa kupata ushindi wa kumwokoa Roselyn. Hii inaleta hakikisho kuwa wanawake wakiungana kupigania asasi zinazowanyanyasa hawana budi kushinda na hivyo ukumbozi wao kupatikana. Misimamo mikali ya dini na utamaduni kumdhulumu mwanamke inapaswa kukomeshwa kwani kwa sasa imepitwa na wakati. Mwanamke na mwanamume wanafaa wawekwe katika mtazamo sawa ili unyanyaswaji wa mwanamke ukomeshwe pia.

### 2.19.4 Ushirikiano kati ya Jinsia Zote

Kuna haja ya jinsia zote za kiume na kike kuja pamoja na kushirikiana katika ubainishaji na ukombozi wa mwanamke. Si wanaume wote wenye nia mbaya katika riwaya hii juu ya ukombozi wa mwanamke. Mwandishi anamtumia Cedric Mwambe kama mmoja wa wanaume wenye nia safi kuhusu mwanamke. Cedric anampongeza Susan kwa kumaliza hatua ya pili katika mfumo wa elimu. Maongezi yake na Susan yanaonyesha kuwa anamtakia Susan mambo mema hata ajiunge na chuo kikuu.

> *Utashindwa vipi kufika University, it is so simple a thing.* (uk 127)

Cedrick baadaye katika chuo kikuu cha Nairobi, anamwalika Susan pamoja na wasichana rafikize katika dhifa ya kusherehekea siku yake ya kuzaliwa. Hii ni ishara kuwa mwanamume ameshatambua thamani ya mwanamke na kushirikiana naye. Hali kama hii ya kumtambua mwanamke ni hatua nzuri ya kupatikana kwa ukombozi wake. Isitoshe, katika mwisho wa riwaya tunaona ushirikiano mkubwa kati ya Mary, Susan na dada zake katika kumrudisha Roselyn nyumbani baada ya kufukuzwa na babake.

Sylvester (1994: 50) anazungumzia wanamfenisti wa kiharakati kule nchini Uingereza wanaoamini kwamba mikakati ya wanawake ya kutafuta nafasi na kujifasiria ukandamizwaji na kuunda mshikamano ni muhimu katika ukombozi wa wanawake wengine. Hapa wanaukabili ushikamano wa wanaume wakandamizaji kwa juhudi za kutafuta na kukomesha kiini cha udhalimu wa wanawake kwa taasubi za kiume.

### 2.19.5 Hitimisho

Katika sura hii tumeweza kuona jinsi msanii alivyoonyesha matumizi mabaya ya dini yanavyochangia kumkandamiza mwanamke. Tamaduni za kijadi pamoja na dini zimekuwa ndizo usuli wa unyanyaswaji wa mwanamke. Richard kufukuzwa na nyoka inaashiria kuwa utamaduni hubakia katika utawala wa jamii kuliko dini. Elimu ya Susan imemtia ujasiri wa kumkosoa Richard aliyeshikilia dini huku anashindwa kuwapa binti zake malezi ya

kuwafaa baadaye. Malezi ya Richard kwa watoto wake yaliongozwa na kihoro cha kuingilia mambo yanayovunja kaida za kidini huku akipuuza nguvu za kitamaduni ya jamii yake.

# SURA YA TATU

# UBAINISHAJI WA MWANAMKE NA UKOMBOZI WAKE KATIKA *DHARAU YA INI* (2007)

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inajadili namna mbalimbali ambazo wanawake hudhulumiwa katika jamii tunayoipata katika riwaya hii. Tutaonyesha jinsi utamaduni unaouegemea upande wa jinsia ya kiume na unatumika kama silaha ya mwanamume kumdhulumu mwanamke. Hata hivyo mawazo ya mwandishi katika riwaya hii yameenda hatua mbele zaidi juu ya ubainishaji na ukombozi kamili ya mwanamke. Katika *Nguvu ya Sala* tunaona jinsi mwanamke anavyoanza kupata elimu na matokeo kamili ya elimu hiyo yanadokezwa kupitia Lila na Derby. Tuliangalia pia asasi nyingine mbalimbali ambazo bado zinaonekana kama changamoto katika ukombozi wa mwanamke. Katika kufanikisha madhumuni ya sehemu hii, tulijikita katika riwaya ya Wamitila ya *Dharau ya Ini* (2007).

## 3.1 Muhtasari wa *Dharau ya Ini*

Riwaya hii inammulika mhusika mkuu, Lila, ambaye tunaambiwa kuwa ameelimika hadi chuo kikuu. Baadaye anaajiriwa kama mwandishi wa habari katika Shirika la Habari la Mpapure jijini K'tambasye. Kupitia sauti yake, Lila akiwa ndiye msimulizi wa hadithi hii, tunapata kujua kuwa alifiwa na babake,

Keli, angali mtoto mdogo. Anapomaliza masomo yake na kupata kazi, Lila hawezi kuikumbuka sura ya babake.

Hadithi inaanza Lila akionyesha hamu ya kutafuta alikozikwa babake. Tunajulishwa baadaye kuwa, nia yake kuu ni kutanzua utata wa kupotea kwa ardhi iliyoachwa na babake. Mumba, mamake Lila, anamwonya dhidi ya hatua hii kwa kummithilishia na hali ya kuchezea bumba la nyuki. Hata hivyo, mamake anamshauri amwone Mzee Mbulu ambaye ndiye angemfichulia mengi kuhusu azma yake hiyo.

Ardhi ya Mzee Keli, tunajulishwa hadithini, kuwa ilinyakuliwa na Kivu, babake Munene, kwa njia haramu ya kumtuma Mzee Kiloo kumuua Keli. Ardhi yenyewe ikarithishwa Munene ambaye amekuwa mkinzani wake Lila katika harakati zake za kutafuta haki yake.

Lila anafanya safari kadha za kulitafuta kaburi la babake, marehemu Keli. Njiani anapokaribia mji wa Munene, anaukabili Mlima wa Mwanamke huku akitafuta mastakimu ya Mzee Mbulu ambaye pia tunajulishwa kuwa ni babu yake Lila mzaa baba.

Tunakumbana pia na Munene, mzee tajiri mwenye wake watatu; Kasina, Katumbi na Debora. Munene anapendelea wakeze wamzalie mtoto mvulana.

Mwanamke anayeshindwa kuyatimiza matakwa haya anatelekezwa. Katumbi na Kasina wanafikwa na masaibu haya. Ni Debora pekee anayesalia anapomzalia mvulana anayeitwa Master John. Munene alipokuwa mfanyakazi katika shirika la reli la *African Railways* anawashangaza watu wengi kwa kupata utajiri wa ghafla licha ya mshahara wake mdogo. Munene anakuwa na uwezo mkubwa wa kifedha na kununua ardhi kubwa na kufungua biashara katika soko moja kijijini kwao.

Kama ilivyofanyika kwa Lila, Munene naye anafiwa na mzazi, kwake akiwa ni mamake, akiwa na umri wa miezi kumi tu. Anatumia jina la utani, "Shujaa wa Kifaru" kutokana na kisa cha babu yake kuuliwa na kifaru zamani. Isitoshe, Munene anapatikana akinyonya maziwa ya mamake akiwa mfu. Babake, Kivu, alikwa chifu kijijini kwao. Lila anapojiingiza katika harakati za kutafuta ardhi yao, Munene naye anatafuta uongozi wa kisiasa kwa kugombea uenyekiti wa chama tawala katika tarafa yao. Anapogundua kuwa Lila anajishughulisha na uchunguzi wa kashfa serikalini, Munene anamwonya akome kuingilia mambo yatakayomtia matatani.

Lila anashirikiana na mwanamke mwenzake kazini anayeitwa Derby. Wanapewa jukumu la kuchunguza na kutayarisha ripoti kuhusu matatizo ya watoto wa kike katika mataa wa Madongoporomoka ulioko K'tambasye. Ripoti ya kwanza inachapishwa siku iliyofuatia ambayo ilikuwa siku ya

kimataifa ya watoto. Derby na Lila wanatekwa nyara na kuachwa siku kadha baadaye kuhusiana na habari waliyoichapisha. Habari hii vile vile inafichua kashfa ya ugavi wa viwanja kule kule Madongoporomoka.

Ripoti zilizotumwa katika Shirika la *Amnesty International*, shirika la kutetea haki ya binadamu ulimwenguni, zinapelekea ujumbe wa wataalamu wa Shirika la Kifedha na Benki ya Dunia kutumwa nchini. Wachunguzi hawa wanakuja kufuatilia ili ibainike iwapo serikali imeshatekeleza mapendekezo ya kukabiliana na ufisadi kama yalivyofichuliwa magazetini. *The Paris Club* inasitisha misaada yote ya kifedha na Benki ya Dunia inafuatia kwa hatua ile ile.

Munene anakumbwa na matatizo mengi, mara fuvu la kichwa, mara anamwona mtu aliyevaa mavazi yake, mara ndoto za kutisha na kisha ugonjwa wa ajabu unaomuua. Sadfa inatokea kuwa Munene anapokufa, Lila naye anafaulu kufichua stakabadhi zilizofukiwa ardhini karibu na kaburi la Keli babake. Wakati huo huo fuvu la babake lililopotea kutoka kaburini linarudishwa kaburini kwa sherehe kubwa na wazee wa jadi.

### 3.2 Mapendeleo kwa Jinsia ya Kiume

Jamii ya riwaya hii inatawaliwa na taasubi za kiume. Licha ya kuwa Lila na Derby wana upeo wa juu wa elimu, wanakumbwa na matatizo kazini kwa

sababu ya jinsia yao. Makhanu anapewa ukuu wa kitengo cha habari kwa kuwa ni mwanamume japokuwa elimu yake ni ya chini ikilinganishwa na ya wanawake hawa wawili.

Munene ni mwanamume mwenye wake watatu; Kasina, Katumbi na Debora. Munene anataka wake zake wamzalie wavulana pekee na sio wasichana. Anawatelekeza Kasina na Katumbi wanaposhindwa kupata mtoto wa kiume. Debora anabakia kwa kuwa amemzaa mtoto mvulana, Master John. Katumbi pamoja na elimu yake, kwake Munene, haifai kitu ikiwa hawezi kumzalia mtoto wa kiume.

Katika jamii hii, urithi wa mali ni kwa upande wa mwanamume pekee. Keli anapokufa hakumwachia mkewe Mumbe vyeti vya kumiliki ardhi kwa vile mwanamke hahusishwi na umilikaji wa mali. Kwa vile hakuwa na mtoto wa kiume, alizifukia stakabadhi za kumiliki shamba ardhini kabla ya kifo chake. Katumbi anakosa utetezi wa wazee alipotaka apewe sehemu ya ardhi ya Munene.

> *Wote walichojua ni utamaduni na desturi tu – watatu walithubutu hata kumkumbusha kuwa alikuwa na watoto wa kike wasiorithi ardhi* (uk.39).

Simone de Beauvoir (1949:67) naye anaonekana kugusia ubaguzi huu anaposema kuwa mume akifa pasipo kuacha wasia, serikali ilichukua mali yote na kumwacha mjane bila kitu. Kwa mujibu wa Toril Moi tunaambiwa kwamba unyanyaswaji wa mwanamke humnyima mwanamke huyo uhuru wake kupitia dhuluma za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiitikadi (Moi 2002:178). Hatua kama hizi ndizo zinazopelekea mwanamke kubakia katika dhiki ya kunyanyasika na jinsia ya kiume.

Jinsia zote zinafaa zichukuliwe sawa ili mwanamke na mwanamume wawe na nafasi sawa katika jamii. Mawazo haya ya kibaguzi ni mambo yaliyopitwa na wakati na humzuia mwanamke kufikia ukombozi wake kikamilifu.

### 3.3 Tamaduni za Kijadi na Ubainishaji wa Mwanamke

Mwanamke ni mtumwa wa mitazamo inayotokana na utamaduni. Kinachoshangaza ni kuwa imani hizi zinaendelezwa hata na wanawake wenyewe. Kasina anaamini kuwa jaala ya kuvunjika kwa ndoa yake na Munene, ilitokana na laana ya ukoo wake wa Koyo. Mawazo haya yanamfanya Kasina ateseke katika nafsi yake hadi anapofariki. Tuanona kuwa utamaduni unamfanya mwanamke asiwe na thamani pasipo kuolewa na mwanamume. Imani kama hizi zinaoana na maoni ya Millett (1970:67) kuhusu wanawake.

Anadai kuwa kanuni za jamii zinampokonya mwanamke haki zake za kibinadamu katika kipindi chote anapoolewa.

Kasina na Debora ni wanawake wanaotawaliwa na hisia za kishirikina. Wakati Kasina anaamini kuwa ndoa yake na Munene imevunjika kwa kufanyiwa uchawi na Debora (anaelekea kusahau suala la ukoo wake hapa). Wazo kama hili linapatikana pia katika kazi ya utafiti iliyofanywa na SIDA. Kuna imani za kishirikina zinazowakumba wanawake wengi wa Afrika kwamba wake wadogo za waume zao hutumia dawa kuwadhibiti waume zao hasa katika ugavi wa rasilimali zilizopatikana kabla ya wao (wakewenza) kuolewa (SIDA 2009:66). Naye Debora anaamini kuwa ugonjwa wa Munene umetokana na uchawi wa Mzee Mbulu, alipotupa fuvu katika mji wao.

Kwa msingi huu huu wa imani za kitamaduni, Mumbe anachelea kumfunulia Lila suala kuhusu ardhi yao kwa imani kuwa ni jukumu la mwanamume. Hii ndiyo sababu anamtuma Lila kwa Mzee Mbulu ambaye kwake ndiye anaweza kushughulikia urithi wa ardhi.

Mwanamke pia anatumika kama chombo cha kutimizia imani za mila na desturi. Wanza anaolewa na King'o akiwa mzee kwa kuwa ni mwiko kwa mwanamume kufa bila mke.

Imani hizi za kitamaduni zinamzuia mwanamke kuitawala nafsi yake. Anaendelea kunyanyasika katika nafsi yake na kushindwa kufikiria anavyoweza kujikomboa kutokana na utawala wa kibabedume uliokita mizizi katika jamii. Mila hizi zinazomdhalilisha mwanamke zinafaa zitupiliwe mbali ili ubainishaji na ukombozi wake upatikane. Sheria hizi zimeundwa na wanaume kama tunavyoelezwa na Fox-Genovees (1991:57), kuwa wanaume ambao wametawala katika sheria wamezitengeneza kulingana na mahitaji yao. Anaendelea kufafanua hali hii kwa kudai kuwa thamani za mwanamume zilitawala huku mwanamke akichukuliwa kama mwakilishi wa malezi; mtunzaji na mwenye huruma huku mwanamume akihusishwa na uhuru, ushindani na wema.

### 3.4 Ukatili Dhidi ya Mwanamke

Mwanamke amesawiriwa katika riwaya hii kama kiumbe wa kupigwa na kudhibitiwa kimabavu. Udhalimu huu unamfanya mwanamke aonekane kama mtumwa mbele ya mwanamume.

Munene anampiga Katumbi na kumfukuza kwa kukataa kuendelea kuzaa hadi mvulana atakapopatikana. Wazo hili linapata uungwaji mkono kuwa haki ya kujiamulia kiuchumi na uwezo wa kuzaa hutegemea ridhaa ya mwanamume. Mwili wa mwanamke huchukuliwa kama miliki ya mume wake (SIDA 2009:18).

Kasina anapigwa kwa kosa la bintiye, Wanza, kwenda kwa Munene kutetea kufungwa kwa mumewe King'o. Debora naye anapigwa na Munene kwa kumkosoa juu ya kutokuwa mwaminifu katika ndoa. Munene anampiga Kasina, mamake Yunga, pale anapojaribu kujinasua alipombaka siku ya sherehe za uhuru. Tunawaona Lila na Derby, licha ya kuwa wanawake wa tabaka la juu kufuatia uwezo wao wa kielimu, wanatekwa nyara na kupigwa kwa kuikosoa serikali. Daima mwanamke anaishi katika mazingira ya ukatili na dhuluma za mwanamume.

Ukatili kama huu dhidi ya wanawake ni dhihirisho kuwa desturi za kijamii zinamwonea mwanamke. Huku ni kumfedhehesha mwanamke na kumnyima hadhi ya kupigania ukombozi wake awe sawa na mwanamume. De Beauvoir (1949:136) anasema kuwa wanaume daima wanawadhibiti wanawake mikononi mwao. Kumpiga mwanamke ni jambo la zamani ambalo sasa linafaa lisahaulike ili mwanamke akombolewe.

Mwanamke hapigwi tu bali anaonewa na kutukanwa vile vile. Vyombo vya dola vinamtumia mwanamke kumtukana mwanamke mwenzake matusi yanayotajwa na msimulizi wa riwaya hii kama "matusi ya nguoni". Lila anapata matusi ya nguoni kupitia askari wanawake anakozuiliwa korokoroni.

Anapoamrishwa na askari atoke garini anapotupwa katika msitu wa Nyirima, anatukanwa.

*Mjinga toka nje!.....*

*Mwanamke ni nini katika nchi hii?* (uk 208/209)

Dharau kama hizi anafanyiwa mwanamke kwa msingi wa jinsia yake. Ni bora jamii ibadilishe desturi ya kumwonea mwanamke kwani anahitajika kukombolewa na kuwa na haki sawa naya mwanamume.

### 3.5 Umaskini na Mwanamke

Umaskini ni hali ya kutokuwa na mali au hali ya ufukara. Umaskini wa mwanamke unatokana na vizuizi alivyowekewa na jamii kuhusu umilikaji wa mali. Badala yake mwanamke anafanywa sehemu ya mali ya mwanamke, Millett (1970:67).

Msichana anayemfanyia Debora kazi anakatizwa masomo kwa ukosefu wa karo. Mamake Debora, Savethi, anaajiriwa na Kivu na kisha kurithishwa Munene kwa sababu ya umaskini. Umaskini ndio unaomfanya Kasina afadhaike juu ya kutelekezwa na Munene. Binti zake wanaenda jijini kujitafutia riziki za kumkimu mama yao.

Mwandishi anatumia umaskini huu wa mwanamke kuelezea hali ya kuwa chanzo cha kunyanyaswa kwake ni kuwa mali ni milki ya mwanamume. Jessica anafanya ukahaba jijini K'tambasye kwa kuwa hana uwezo wa kiuchumi na ndiyo sababu anaangukia mkononi mwa Munene. De Beauvoir (1949:513) anasema kuwa mwanamke kwa umaskini wake hulazimika kujiingiza katika hatia ya kuuza mwili wake ili kuficha makosa ambayo wenzake huamini hayawezi kusameheka. Suala hili linatawala Afrika nzima kwani itikadi iliyokita mizizi kuwa mwanamke hana mamlaka juu ya rasilimali (SIDA 2009:63).

Hali hii ya umaskini unamfanya mwanamke kuwa mtumwa wa mwanamume. Kumkataza mwanamke kurithi mali ni kumfanya maskini na hivyo kumkandamiza na kumzuia kupata ubainishaji na ukombozi wake kwa kumnyima uwezo wa kiuchumi.

### 3.6 Mwanamke Kama Chombo cha Burudani

Baadhi ya wanaume katika riwaya hii, kama vile Waziri Kisingo Kanda na Munene, wanamchukulia mwanamke kama chombo cha kujistarehesha ili kutoshelezea ashiki ya miili yao. Waziri Kisingo Kanda anamshauri Munene asizoee mwanamke mmoja tu.

*Bwana wee, ukikaa na mtu yule, unaamka asubuhi, unamwona hajanawa uso na nywele kuipeleka saluni.... Kabla mdomo kutiwa lipstick, bado kinywa kinanuka tombovu, macho kutiwa wanja, kope kupakwa mkahale! Ehh wacha!* (uk 83).

Kauli kama hii inamdunisha mwanamke na kumfanya aonekane kama chombo tu cha burudani. Munene anapobadilisha jina la Jessica na kuwa Jessica Baby, tunapata picha ya mwanamume kumgeuza mwanamke kama kifaa cha kujipumbaza akiwa mbali na mkewe.

Munene anambaka Kasina, mamake Yunga, siku ya sherehe za uhuru wa nchi yao ishara kuwa mwanamke ni sehemu ya chombo cha kujiburudisha siku kama hii. Wazazi wake Kasina wanapolalamika kwa chifu Kivu (babake Munene) kuhusu dhuluma hii, badala ya kumwadhibu, Kivu anamfurahia Munene na kumwona kama jogoo anayekuwa kisawasawa. Mapambo na mtindo wa mavazi ya mwanamke yanamfanya mtumwa na mnyonge mbele ya uchu wa kiume, de Beauvoir (1949:513).

Tendo la kumgeuza mwanamke kifaa ni kumnyima haki yake ya kuwa binadamu. Hali kama hii ndiyo inayowafanya wanawake kuamua kujijumuisha

katika siasa ili kumaliza utumwa na kujitia shime ya kupigania ukombozi wa mwanamke Millett (1970:80).

### 3.7 Mwanamke Kama Kiwanda cha Kutengenezea Watoto Wavulana

Mtunzi anatujulisha jinsi Munene anavyomlazimisha Katumbi kuendelea kuzaa hadi mvulana apatikane.

> *Unaweza kuzaa watoto idadi yoyote mradi una uwezo wa kiuchumi na huo ninao.* (uk 38)

Katumbi anakataa mwili wake kugeuzwa mgodi wa kuchimbulia wavulana. Munene anakasirika na kumpiga kwa kutotii amri yake kama mumewe. (uk 38). Kipigo hiki kinatokana na itikadi inayoendelezwa na ubabe wa mwanamume barani Afrika kuwa mwanamke anatakikana kumheshimu mumewe (SIDA 2009:87).

Debora anaolewa na Munene baada ya Kasina na Katumbi kukosa uwezo wa kumzalia Munene watoto wa kiume. Wazo hili ni la tangu jadi kwani wanaume wa jamii nyingi ya Afrika huoa wanawake zaidi wasiporidhishwa na uzazi wa wake wa kwanza ili wapate idadi ya watoto wanaowahitaji (SIDA 2009:66). Hii ni ithibati ya mwanamke kugeuzwa kiwanda cha kuzalisha watoto wavulana.

*Unazaazaa wasichana tu, hujui kuzaa watoto wa kiume wewe? Nitaoa mwanamke anayejua kuzaa watoto wa kiume.* (uk.36).

Imani na mtazamo wa kuwa mvulana ndiye mrithi wa mali inamfanya mwanamke abaguliwe. Ni lazima ikubalike kuwa watoto wa jinsia zote ni sawa. Kwa hivyo, mwanamke ni vyema achukue msimamo kama ya Katumbi ajikomboe kutoka katika dhuluma za wanaume wa kumfanya kama chombo tu.

### 3.8 Uhafidhina wa Wazee na Ubainishaji na Ukombozi wa Mwanamke

Uhafidhina ni hali ya kutobadilisha mawazo, itikadi au imani ya kijadi kuhusu masuala fulani ya kijamii. Mwandishi anatujulisha kuhusu wazee wanaoona kuwa imani za kijadi ni sharti zibakie pale pale. Wazee wa ukoo wanakataa dai la Katumbi kutaka kurithi sehemu ya ardhi ya mumewe (uk.39).

King'o anajaribu kumpiga mkewe Wanza ili kupinga hatua ya Wanza kumfedhehesha mbele ya wageni wake kinyume na desturi ya kitamaduni kuwa mume hawezi kudhibitiwa na mkewe. Ingawa anashindwa kumpiga Wanza na badala yake kupigwa yeye, tunapata picha ya ubabedume wa mwanamume kumkandamiza mwanamke. Wanza anachukua hatua nzuri ya kukomesha ukatili wa mumewe kwake na hii ni mfano mzuri wa kuigwa na

wanawake wengi ili kukata minyororo ya ubabedume unaowanyima ukombozi wao.

## 3.9 Juhudi za Kumbainisha na Kumkomboa Mwanamke

Neno ubanishaji limetumika mara kadha katika tasnifu hii. Kulinga na na Kamusi ya Visawe (1998) neno ubainishaji lina maana kadha; dhihirika, onyesha tofauti, fafanua, fichua, fumbua, sherehi, pambanua, tongoa na eleza. Maana hizi zina karinbiana sana. Kamusi ya TUKI (2006) nayo inaieleze neno ubainishaji kama ona na tambua. Maana tuliyokusudia ni ya TUKI. Kwani mwanamke anafaa aonekane mwenye sifa na heshima sawa na mwanamume. Kadhalika mwanamke ni sharti atambuliwe na athaminiwe katika mambo yote ya kijamii. Yote haya kwa pamoja ndio yanapelekea ukombozi kamili wa mwanamke.

### 3.9.1 Ushirikiano kati ya Wanawake na Wanawake

Juhudi za ubainishaji na ukombozi wa wanawake unahitaji ushirikiano na ushikamano wa hali ya juu. Lila na Derby walishirikiana katika kuchunguza matatizo yanayowakumba watoto wa kike katika mtaa wa Madongoporomoka jijini K'tambasye. Ingawa shughuli hii inatatizwa kisiasa na wanaume kama Waziri Kisingo Kanda na Munene, hii ni hatua ya kuwatambua na kuwakomboa wanawake kutokana na shida wanazokumbana nazo maishani.

Kama si ushirikiano waliokuwa nao Lila na Derby, hawangepata nguvu za kuwawezesha kutamatisha uchunguzi huu wao.

Katumbi kwa kushirikiana na mwanasheria mmoja wa kike, anafaulu kubadilisha jina lake kutohusishwa na la Munene ambao amekwishatengana naye. Sasa anaitwa Ms Immaculate Katumbi badala ya kuitwa Mrs Ken. Hili ni wazo lisilobishika kwani ukweli kuwa duniani kote ikiwemo bara la Afrika, wanawake walioolewa wengi wao huwa na mjina ya wanaume katika vyeti vyao vya kumiliki ardhi, nyumba na mali nyingine (SIDA 2009:61).

Ushirikiano huu si mbaya kuwahusisha pia wanaume ambao wanatambua umuhimu wa mwanamke katika maendeleo ya jamii. Ili kumrudishia haki ya kumiliki ardhi iliyoachwa na Keli babake, Lila anashirikiana bega kwa bega na Mzee Mbulu anayemtia shime asiogope safari ndefu na ngumu aliyoianza. Lila pia kwa ushirikiano wake na mwalimu wake wa zamani, Profesa Veritas Mbogo, anafaulu kupata ripoti zaidi kutoka matbaa ya chama na serikali. Profesa Mbogo anamsaidia Lila kuingia *Central Archives* ambamo alipata habari zaidi za kumsaidia katika uchunguzi wa ugavi wa ploti mtaani Madongoporomoka.

Mwandishi anaelekea kuidokezea jamii kuwa umoja ni nguvu. Kupitia kwa ushirikiano sio tu wa wanawake wenyewe bali pia ushirikiano wao na

wanaume, wanawake wanaweza kufaulu dhidi ya unyanyaswaji wa wanaume wasiowathamini. Ushirikiano wa wanaume wenye mtazamo mzuri kuhusu wanawake unaweza kufanikisha lengo la wanawake kujikomboa. Juhudi kama hizi zinakabiliana na ushikamano wa wakandamizaji wanaofanya miili ya wanawake kama mahali panapodhibitiwa na wanaume, Sylvester (1994:50).

### 3.9.2 Wanawake Kujiendeleza Kielimu

Kulingana na de Beauvoir (1949:110) bila elimu, uwepo wa mwanamke ni vigumu kutambulika. Elimu waliokuwanayo Lila na Derby ndiyo inawawezesha kufikia tabaka la juu. Lila, Derby na Katumbi ni wanawake wenye elimu inayowafanya waweze kujikimu bila kumtegemea mwanamume. Jambo linalotia aibu ni kwamba, iwe elimu au bila elimu, na kuwa mwanamke awe na uwezo wa kujipatia mali au hapana, bado atatumikishwa na mumewe (SIDA 2009:67). Derby ana gari, Lila anafuatilia urithi wa shamba huku Katumbi akijinunulia shamba baada ya kufukuzwa na mumewe Munene na bado hawajaponyoka kutoka kwenye udhalimu wa wanaume.

Kwa kufaulu katika elimu na kuwa mwalimu, tunamwona Katumbi akifaulu kuwaelimisha binti zake na vile vile kufahamu kuwa kuna sheria aliyoitumia kubadili jina lake asiitwe Mrs Munene.

> *Binti yake wa kwanza alifuzu vizuri katika mtihani wa darasa la sita. Kitinda mimba alikuwa katika darasa la tano.* (uk 49).

Mwandishi anaelekea kupendelea elimu ya mwanamke kwa kuvitaja vitabu alivyovisoma Lila. Vitabu hivi ni kama vile *The Place of Dreams* cha Ismail Kadare, *Who Killed Polomini Molero?* cha Maria Vargas Llosa, *The President* cha Miguel Asturia, *The Joke* cha Milan Kundera, *Fire Under the Snow* cha Palden Gyatso. Anuani za vitabu hivi zinaakisi mada za kimapinduzi ambazo zinaonekana ndizo zilizochochea ari ya Lila kuwa mkakamavu katika kupigania haki yake na ya wanawake wengine.

Elimu ya Derby iliyompeleka kusomea Marekani ilimpa tajiriba nzuri ya kumpa mwamko katika mapambano ya kumkomboa mwanamke. Baada ya Makhamu kuachishwa kazi ya ukuu wa kitengo katika Shirika la Habari la Mpapure, Derby ndiye aliyepandishwa cheo na kuchukua nafasi hiyo. Uelewa wa Lila wa lugha ya Kifaransa (uk 216) ulimpa uwezo wa kusoma vitabu vingi vilivyoandikwa katika lugha hiyo na kupata maarifa zaidi yaliyompatia uwezo wa kuwa mtetezi wa wanawake.

Kulingana na ithibati inayopatikana katika riwaya hii, tunaona kuwa wanawake wakiwa na elimu wana uwezo sio tu wa kujikomboa kibinafsi na

kijinsia, bali pia kushiriki katika kuondoa maovu katika jamii kwa ujumla. Millett (1969:74) akirejelea awamu ya kwanza ya mageuzi kuhusu jinsia ya wanawake anasema kuwa uhuru wa kundi lo lote linalodhulumiwa, elimu ndio uliopewa kipaumbele.

### 3.9.3 Mchango wa Mashirika ya Ndani na Nje ya Nchi katika Ubainishaji na Ukombozi wa Mwanamke.

Ukombozi wa mwanamke na ubainishaji wake unahitaji mchango wa mashirika ya ndani na nje ya nchi hasa yanayojishughulisha na haki za kibinadamu. Ripoti kuhusu dhiki zinazowakumba watoto wa kike mtaani Madongoporomoka inayavutia mashirika ya umma na ni hatua kubwa katika ukombozi wa mwanamke. Mashirika mawili yameomba idhini ya kuchapisha ripoti hizo ili zitumiwe katika makongamano ya kimatiafa (uk.116). Kutokana na uwezo wao wa kifedha na uwezo wao wa kufikia sehemu kubwa ya dunia, ni ishara kuwa juhudi za kumkomboa mwanamke ni suala la ulimwengu mzima.

Wanaume kama Sylvestein Makhamu wanaona ripoti kama hizi kuwa na ufeministi usiofaa na kuwa na mielekeo ya kuwapendelea wanawake wanafaa kupigwa vita, wasiwe kikwazo katika ubainishaji na ukombozi huu.

Shirika la Haki za Kibinadamu la *Amnesty International* limeongeza kasi ya ukombozi wa mwanamke. Shirika la Ulimwengu la Kifedha pamoja na Benki ya Dunia kwa kuitambua kazi iliyofanywa na wanawake, na kuwatuma wajumbe wao kuja kufuatilia utekelezaji wake, ni hatua inayotia moyo. Juhudi hizi za kimataifa zinaleta matumaini makubwa katika bidii za wanawake za kukomboa jinsia yao. Lazima ikumbukwe kuwa, ripoti iliyobeba kadhia ya ufisadi serikalini, ilihusu dhiki ya watoto mitaani vile vile. Wanawake wanaungwa mkono ulimwenguni kwa hivyo wasikate tama katika juhudi zao za kujikomboa kwani ulimwengu mzima u radhi kushikamana nao.

### 3.9.4 Mwanamke na Asasi ya Ndoa

De Beauvoir (1949:105) anasema kuwa wanawake walioolewa bila hiari yao hutendewa kama watumishi. Mwanamke kuwa mfungwa katika ndoa ni kati ya maoni yaliyopitwa na wakati. Usemi kuwa '*mume ni mke wa kwanza*' unamfanya Kasina amtegemee mume aliyeacha kumjali zamani. Jamii nyingi za Afrika hudai kuwa dhiki katika ndoa haimaanishi bahati mbaya bali ni sehemu muhimu katika maisha ya mwanamke. Kuumia na kuteseka ni kawaida maishani. Uwezo wa kuvumilia machungu na dhiki ndio utambuzi wa maadili (SIDA 2009:106). Mawazo haya kwetu ni ya kupotosha na hayana msingi wo wote katika maisha ya mtu awaye yule. Matumaini kuwa siku moja Munene atarudi yamemfumba macho na kumfanya ateseke kwa maradhi ya moyo hadi anakufa.

Desturi hizi za kijadi ni lazima zisahaulike kwani inapaswa ieleweke kuwa mwanamke si lazima aolewe ndipo awe na maisha mema. Derby na Lila wanaongoza maisha ya ufanisi licha ya kuwa hawajaolewa. Katumbi baada ya kutengana na Munene alinunua ardhi na kuwaelimisha binti zake kwa kutegemea jasho lake binafsi. Millett (1969:99) akinukuu mawazo ya Mill kuhusu ndoa, anadai kuwa mwanamke hunyimwa kila kitu maishani isipokuwa kile cha kubakia mhudumu wa mwili wa mtawala wake (mwanamume). Anaongeza kuwa ingawa mume anaweza kumtaliki mkewe, mke huyo hawezi kumponyoka.

Genz na Brabori (2009:52-53) nao wakimnukuu Friedan, wanasema kuwa wanawake wa nyumbani wapo katika hatari sawa na mamilioni walioelekea kifo katika kambi ya mateka ya vita. Kasina na Debora kwa kung'ang'ania kubakia wake za Munene kwa sababu ya mali aliyokuwa nayo kunawafanya waonekane wafungwa na watumwa mbele ya mwanamume.

Ni heri wanawake watafute njia bora za kujitegemea kuliko kuvumilia dhuluma zinazokandamiza haki zao katika ndoa. Mfano wa Katumbi kuendelea kivyake baada ya kutelekezwa na Munene, ndio unafaa kuigwa na wanawake ili wafikie upeo wa ukombozi wao.

### 3.9.5 Ishara za Kimaumbilie na Ukombozi wa Mwanamke

Mtunzi anatumia Mlima wa Mwanamke kama taashira ya matumaini katika ukombozi wa mwanamke. Lila anaposafiri kufuatilia mirathi yake tunamwona kila wakati akilitazama jabali hilo. Taswira ya jabali kudondokwa machozi ni ishara ya mwanamke anayelilia udhalimu anaofanyiwa na jamii yake mwenyewe.

> *Niliuangalia ule mlima tena na kuyakumbuka yale machozi niliyoyaona siku ile. Machozi ya Mlima wa Mwanamke. Machozi ya mwanamke. Nilitikisa kichwa kisha nikaufuata njia unaotumiwa na watu kwenda kisimani.* (uk 18)

Ugumu na ukubwa wa jabali hili ni ishara kuwa taasubi za kiume zitapondwapondwa na wanaume hao kushindwa katika juhudi zao za kumkandamiza mwanamke. Mwamba huu utaangamiza imani na amali zote za kitamaduni na desturi kandamizi.

Ukoo wa Munene hauli ini. Ini hapa inaashiria jinsia ya kike ambayo imedharauliwa na wanajamii wakiongozwa na mwanamume. Munene kulila ini hospitalini ili kuchangia kuimarika kwa afya yake, ni ishara kuwa wanaume wamejisalimisha na kukiri kuwa mwanamke hawezi kudharauliwa tena. Ini

kumkwamia Munene kooni na kuzidiwa ugonjwa inaakisi ushindi wa kubainika kwa mwanamke na ukombozi wake kwani nguvu za ukandamizaji zimeangamizwa kupitia kufa kwa Munene.

Mwandishi pia anatumia fuvu kama mzimu unaomfuata kila aendapo. Kwanza fuvu ni ishara ya wahenga wa jadi wasiofurahishwa na kutwezwa kwa mwanamke. Inamaanisha kuwa fuvu limsumbualo Munene ni la babake Lila. Siku ya kupatikana kwa stakabadhi maalum ya ardhi ya Keli, inasadifika kupataikana kwa fuvu. Hii ni ishara ya kupatikana kwa ukombozi wa mwanamke. Sherehe za kitamaduni zinazofanywa na wazee pia ni ishara kuwa wazee wanafaa kukoma uhafidhina wa kung'ang'ania mila za desturi baguzi na kuungana pamoja katika kumkomboa mwanamke. Nguvu hizi za kimaumbile ndizo silaha dhabiti anazotumia msanii kuzikejeli mila na desturi za jadi na kuitetea ubainishaji na ukombozi wa mwanamke.

### 3.9.6 Hitimisho

Mwandishi ameonyesha jamii zinazokuwa kikwazo kwa ubainishaji na ukombozi wa mwanamke. Anawatumia wahusika Lila, Derby na Katumbi kama kielelezo mwafaka cha wanawake waliofaulu kupiga vita dhuluma dhidi ya mwanamke. Tumeona vile vile kuwa ukombozi wa mwanamke, hauwezi kutimia bila mchango wa wanaume wenye nia njema kuhusu maendeleo ya wanawake. Mashirika ya jamii nchini na ya kimataifa yamedokezwa kuwa na

mchango muhimu kukomesha maovu na uozo katika jamii. Riwaya hii inaonyesha mabadiliko makubwa ya mawazo ya mwandishi juu ya utetezi wa haki za mwanamke. Hapa amememuumba mwanamke aliyepiga hatua ya mbele kielimu akishindana na mwanaume katika utekelezaji wa maendeleo. Katika riwaya ya kwanza ya *Nguvu ya Sala*, mwanamke bado yupo katika hatua za mwanzo za kujiendeleza.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO NA MAPAENDEKEZO

## 4.0 Utangulizi

Katika tasnifu hii tulishughulikia ubainishaji na ukombozi wa mwanamke kwa kuchukua mkondo wa ufeministi wa kiharakati. Tumetumia riwaya mbili za Wamitila; *Nguvu ya Sala* na *Dharau ya Ini*, ili kupata jinsi mwandishi alivyowasawiri wahusika wake wa kike.

Ufeministi wa kiharakati kama tulivyoelezea hapo juu, ulitufaa kwani unahusu mapinduzi ya jamii ya kike inayokandamizwa na wanaume ili kunyimwa haki zao. Kwa vile mazingira ya kitamaduni katika jamii yanaumba sura ya mwanamke kuonekana kiumbe mnyonge, mwanamke anakumbwa na matatizo chungu nzima ili kufikia ukombozi wake. Taratibu za mifumo ya kiuchumi, kisiasa, kidini na kitamaduni zinatumika sana na jamii kumkandamiza, kumdhalilisha na kumbagua mwanamke. Ni wazi kuwa mifumo hii inayopendelea kuwa mwanamke amtegemee mwanamume, inachangia sana kumfanya mwanamke anyanyaswe, aonewe, adharauliwe na adunishwe na mwanamume. Hali hii inachangiwa na picha ya mwanamke kama chanzo cha uozo katika jamii. Katika muktadha huu, mwanamke amechorwa kama mchawi, muuaji, hali inayofanya jamii kutobadilisha mtazamo wake kuhusu mwanamke. Haya ndiyo mambo ambayo tasnifu hii yanakusudia kuyarekebisha ili mwanamke atambulike na akombolewe.

## 4.1 Matokeo ya Utafiti

Matatizo ya utafiti huu umeshughulikia ubainishaji na ukombozi wa mwanamke. Uchunguzi wetu umetumia riwaya mbili; *Nguvu ya Sala* na *Dharau ya Ini*, zote za Wamitila. Madhumuni yetu yalikuwa kutafiti asasi za jamii zinazochangia ukandamizwaji na unyanyaswaji wa mwanamke. Tulijifunga katika kuikosoa mifumo inayozuia ufanisi wa ukombozi wa mwanamke. Kisha tulikuwa na nia ya kuonyesha kuwa mwanamke akipewa nafasi kama ya jinsia ya kiume, ana uwezo wa kuchangia maendeleo ya jamii kwa kuangamiza uozo unaoangamiza binadamu kwa ujumla. Lila na Derby ndio wamekuwa kielelezo mwafaka cha kutimizia hatua hii.

Nadharia iliyotuongoza ni ya ufeministi wa kiharakati. Wananadharia hii kama vile Virginia Woolf ndio waasisi wa utetezi wa haki za wanawake kazini, nyumbani na katika asasi kama zile za dini. Asasi hizi zimetumiwa kumnyanyasa mwanamke na kumfanya mtumwa wa mwanamume. Kwa kutumia nadharia hii tulionyesha haja ya kumbainisha na kumkomboa mwanamke kama sehemu ya haki ya kutetea haki ya kibinadamu.

Kupitia upimaji wa nadharia tete, imedhihirika kuwa mwanamume humchukua mwanamke kama chombo tu cha kujistarehesha au cha kutumikishwa na si

kama binadamu. Haya yamejitokeza kupitia wahusika kama Munene na Waziri Kisingo.

## 4.2 MapendekezoYetu

Mapendekezo yetu katika riwaya hizi mbili ni kuwa zinahitaji kuhakikiwa zaidi kwa misingi ya nadharia nyingine mbalimbali ili kupata mwangaza zaidi kuhusu mitazamo tofauti inayohusu mifumo ya jamii inavyiwachukua mwanamke.

Hati hivyo kulingana na utafiti wetu, kunahitajika mapinduzi ya itikadi za kijadi zinazomfanya mwanamke kuwa ndiye mtumwa wa tamaduni za jamii. Katika ndoa kwa mfano, imani kuwa mke ni sharti amnyenyekee mumewe huku mume akimwelekezea ukatili, inafaa irekebishwe na kufanya jinsia zote kuwekwa katika nafasi sawa. Kwa hivyo, jamii inapaswa kumtambua na kumkubali mwanamke kuwa ni binadamu mwenye haki sawa na ya mwanamume. Watoto wa kike wasibaguliwe kwa sababu tu ya jinsia yao.

## 4.3 Hitimisho

Suala la mahusiano ya jinsia katika jamii linaonekana kuwa na mvuto sana miongoni mwa wahakiki wa fasihi. Kushughulikiwa kwalo kunahitaji makini ili migogoro inayojitokeza kati ya jinsia hizi mbili imalizike. Fasihi ya Kiswahili inafaa kuupigia upatu suala hili ili kuielimisha jamii kuacha desturi

zilizopitwa na wakati na kuchukua mtazamo unaoifaa jamii ya kisasa, kwa manufaa ya wanajamii wote.

## MAREJELEO


Beauvoir, S (1949) *The Second Sex*. London: David Campbell Publishers Ltd, 1993.

Bell na Offen (1983) *Women, the Family, and Freedom: The Debate in Documents*: Stanford Carlifornia; Stanford University Press

Burhani, Z (1987) *Mwisho wa Kosa*. Nairobi. Longhorn Publishers (K) Ltd.

Eagleton, M (2007) *Feminism Literary Criticism*. London: Longman.

Fishburn, K (1982) *Women in Popular Culture: A Reference Guide*. Greenwood Press Westpoint.

Fox – Fenovees, E (1991) *Feminism Without Illusions: A Critique of Individualism*. London: The University of North Carlifornia.

Gatare (1993) "Dini Katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Genz na Baron (2009) *Post-feminism Cultural Text and Thomas.*_Edinburg: Edinburgh University Press Ltd.

Kweyu (2007) "A Critical Analysis of Patriarchy and Masculinity in Kezilahabi's Rosa Mistika and Kichwamaji." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Kratochvil, L (1980) *African Women: A Select Bibliography*. Cambridge: African Study Centre.

Lugano (190) "Mwanamke Katika Riwaya za Kezilahabi". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mbatia, A. M (2001) *Kamusi ya Fasihi.*_Nairobi: Standard Textbook Graphics and Publishing.

____________(2003) "A Critical Approach to Wamitila's *Nguvu ya Sala.* Hekima Journal of Humanities and Social Sciences." Juzuu la 1 na 2. Haijachapishwa.

Mkangi, K (1995) *Walenisi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mlacha na Madumula (1991) *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Miruka, et al (2003) "FEMNET Training Manual on Gender Based Violence; The African Women's Development and Communication Network. Haijachapishwa.

Mohamed, S.A (1980) *Utengano:* Nairobi: Longhorn Kenya Ltd. – Sasa Sema Publications.

Mohamed, S. M (1983) *Nyota ya Rehema*. Nairobi. Oxford University Press.

Morgan, R (1992) *The word of a Woman*. New York: W.W Norton and Company.

Mutua, M (2007) "Mitazamo ya Vijana na Wazee Kuhusu Ukombozi wa Mwanamke Katika Tamthilia Tatu za Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mwangangi, F. M. (1996) "Uhakiki wa Fani Katika Tamthilia ya Jay Kitsao."

Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu . cha Nairobi. Haijachapishwa.

Ndungo (1985) " Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Njogu na Chimera (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyamberi (1997) "Mwamko wa Mwanamke katika Tamthilia Nne za Penina Muhando." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Ramazanoglu, et al (2002) *Feminism Methodology Challenges and Choices.* London: SAGE Publications.

Sylvester (1991) *Feminism Theory and International Relations in a Postmodern Era.* Cambridge: Cambridge University Press.

Tripp (2000) *Women and Politics in Uganda*: Kampala, Jmae currey Ltd Oxford; The University of the Winsconsin Press Madison

TUKI, (2006) *English – Kiswahili Dictionary*. Dar es Salaam: 3rd Edition. Institute of Kiswahili Research University of Dar es Salaam.

Turshen and Holcomb(1993) *Women's Lives and Public Policy: The International Experience:* Westport, Connecticut; London Greenwood Press.

Umar bin Amini (1251*) Utendi wa Ayubu*. Maelezo mengine hayakupatikana.

Wafula et al (2007*) Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: J.K.F

Wamitila, K. W. (1999) *Nguvu ya Sala*. Nairobi: Longhorn Publishers.

_______________(2002) *Uhakiki wa Fasihi: Msingi wa Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

_______________(2003) *Kamusi ya Fasihi: Istikadi na Nadharia.* Focus Books.

______________(2007) *Dharau ya Ini.* Nairobi: Vider Muwa Publishers Ltd.

______________(2008) *Kanzi ya Fasihi 1: Msingi ya Uchanganuzi* wa Fasihi. Nairobi: Vide – Muwa Stima Printers & Stationers Ltd.